NDAKI YA ELIMU

SKULI YA ELIMU

# UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA STADI ZA KUSOMA NA KUANDIKA KWA WANAFUNZI WA KISWAHILI WA SHULE ZA SEKONDARI WILAYANI NYAMAGABE

**MUKASHEMA CONCESSA**

**Nambari ya usajili: 220018350**

**TASNIFU INAYOWASILISHWA KWA KUKAMILISHA MAHITAJI YA SHAHADA YA UMAHIRI WA ELIMU KATIKA KISWAHILI NA ELIMU YA CHUO KIKUU CHA RWANDA, NDAKI YA ELIMU**

**Agosti, 2022**

# IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, MUKASHEMA Concessa ninathibitisha kuwa kazi ya utafiti huu ni yangu ya asili na hakuna mtu yeyote aliyeiwasilisha kwenye Chuo Kikuu chochote ili apewe shahada au tuzo yoyote ile.



Tarehe : 5 Agosti 2022

# ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyesaini hapa chini, alisaini ili kuthibitisha kuwa kazi ya utafiti hii ambayo ina kichwa cha **"Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika kwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Sekondari Wilayani Nyamagabe** ", limefanywa chini ya usimamizi wake na anapendekeza likubaliwe na Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu kwa ajili ya utafiti.

Dkt. Patrice NTAWIGIRA

(Msimamizi)

Tarehe:08/08/2022

# SHUKRANI

Mosi, shukrani zangu ninazielekeza kwa Mungu aliyenilinda tangu nilipozaliwa na kunipa uwezo wa kutimiza masomo yote ambayo niliyasoma.

Pili, msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt. Patrice Ntawigira afikiwe na shukrani zangu za dhati kwa kunipa mwongozo ulioniwezesha kutimiza kazi ya uandishi wa pendekezo la utafiti na ripoti ya tasnifu hii. Ninamshukuru sana kwa usimamizi wake mzuri pamoja na ushauri alionipa ili kazi hii ya utafiti iweze kukamilika.

Tatu, nataka kumshukuru mume wangu mpendwa Bimenyimana Jean Marie Vianney, watoto wangu wapendwa, Yvette Umugwaneza na mumewe Gashongore Callixte, Iragaba Alain Patrick, Shema Jean Yves, Ishimwe Nadine, Turabayo Eric Gilbert, Tuyishime Jean Paul, Kwizera Robert, Mwizerwa Germaine, Mahoro Laetitia , Cyuzuzo Anitha, ndugu zangu wote, familia ya Nsengimana Léon, familia ya Maniraguha Jean Bosco,familia ya Bwana Gatabazi Bernard, familia ya Bwana Karangwa Prosper na marafiki zangu wote walionisadia katika masomo yangu.

Nne, ninatoa shukrani zangu kwa walimu walionifundisha hasa katika Chuo Kikuu cha Rwanda wakiwemo Dkt. Wallace Mlaga na Bw. Ntawiyanga Sylvain. Walimu hawa wasingelinifundisha, nisingelijua yale ambayo ninayajua hasa kwa lugha ya Kiswahili. Pia, ninawashukuru wanafunzi wenzangu tuliosomea pamoja. Mchango wao wa kunisisimua na kunikuzia akili kupitia mijadala tele tuliyofanya tukiwa chuoni. Ninawashukuru pia  wanafunzi wenzangu Tuyishimire Laurien, Bisamaza Emilien na Bikorimana Donald kwa misaada yenu mlionipatia.

Mungu awajalizie mema.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu mpendwa Bimenyimana Jean Marie Vianney, watoto wangu wapendwa pamoja na ndugu zangu wote. Subira, uvumilivu na motisha na msaada mlionipa uliniwezesha kukamilisha kazi hii ya utafiti.

# IKISIRI

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu la kuchunguza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika MUU kwa wanafunzi wa shule za upili kwenye wilaya ya Nyamagabe nchini Rwanda. Utafiti wetu ulikusudia kukamilisha malengo mahususi matatu yaliyokuwa ni pamoja na kubainisha namna ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari kwenye wilaya ya Nyamagabe, kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika utekelezaji wa MUU kwa shule za sekondari kwenye wilaya ya Nyamagabe na kupendekeza mikakati inayoweza kutumiwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika kupitia MUU kwa wanafunzi wa shule za sekondari kwenye wilaya ya Nyamagabe. Ili kutimiza malengo ya utafiti, utafiti wetu ulikusanya data kupitia mbinu ya usaili na uchanganuzi matini. Wango katika utafiti huu lilihusisha wakuu wa masomo pamoja na walimu wanaofundisha Kiswahili ambao walichaguliwa kutoka kwenye shule teule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe kwa kutumia usampulishaji lengwa. Utafiti huu ulitumia mkabala wa kitamuli. Uchanganuzi wa data pamoja na ufasiri wa data uliongozwa na Nadharia ya Utamadunijamii. Aidha, matokeo ya utafiti wetu yalionesha kwamba walimu wanaofundisha Kiswahili kwenye wilaya ya Nyamagabe hawafundishi stadi ya kusoma na kuandika Kiswahili vilivyo kutokana na utumiaji wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zisizofaa na ukosefu wa uwezo wa kuandaa vilivyo maandalio ya mafunzo yanayolenga kukuza uwezo wa usomaji na uandishi wa Kiswahili kwa wanafunzi. Baada ya matokeo ya utafiti kudhihirisha changamoto zinazokabili walimu wanapofundisha kuandika pamoja na kusoma Kiswahili katika utekelezaji wa MUU kwa shule za sekondari wilayani Nyamagabe ambazo ni ukosefu wa utamaduni wa kuandika na kusoma, upatikanaji na ufanisi wa vifaa vinavyohitajika katika kusoma na kuandika Kiswahili, ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi na uhaba wa walimu wa Kiswahili wenye uwezo, utafiti wetu umependekeza mikakati ambayo walimu wanaweza kutumia na walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili ili kuepuka changamoto zinazokabili walimu wanapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe. Mikakati hiyo ni utumiaji wa TEHAMA, utumiaji wa Andaa- Shiriki na Tafakari, utumiaji wa usomaji na uandikaji gawizwa na utumiaji wa mbinu ya ujenzi wa maarifa. Isitoshe, tasnifu hii inapendekeza kuwa ni lazima walimu, wakuu wa masomo, viongozi wa shule na wadau wengine wa sekta ya elimu waungane mkono kwa madhumuni ya kuimarisha shughuli za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwenye ngazi zote za elimu katika nchi ya Rwanda.

# YALIYOMO

IKIRARI NA HAKIMILIKI ........ ii
ITHIBATI YA MSIMAMIZI ........ iii
SHUKRANI ........ iv
TABARUKU ........ v
IKISIRI ........ vi
YALIYOMO ........ vii
ORODHA YA VIFUPISHO ........ 0
UTANGULIZI ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 1
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 4
1.3.1 Lengo la Jumla ........ 5
1.3.2 Malengo Mahususi ........ 5
1.4 Maswali ya Utafiti ........ 6
1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 6
1.6 Mawanda ya Utafiti ........ 7
1.6.1 Mawanda ya Kimaudhui ........ 7
1.6.2 Mawanda ya Kijiografia ........ 7
1.6.3 Mawanda ya Kimuda ........ 7
1.7 Vikwazo vya Utafiti ........ 8
1.8 Mpangilio wa Utafiti ........ 8
SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO ........ 9
2.0 Utangulizi ........ 9
2.1 Dhana ya Stadi ya kuandika ........ 9
2.2 Dhana ya Stadi ya Kusoma ........ 13
2.2.1 Aina za usomaji ........ 14
2.2.2 Mbinu za Kusoma ........ 16

2.2.3 Madhumuni ya Kusoma ........ 17
2.3 Changamoto Zinazokabili Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusona na Kuandika ........ 18
2.3.1 Ukosefu wa Utamaduni wa Kusoma na Kuandika ........ 19
2.3.2 Ukosefu wa Vifaa Vinavyohitajika katika Kusoma na Kuandika ........ 20
2.3.3 Ukosefu wa motisha miongoni mwa Wanafunzi ........ 21
2.3.4 Uhaba wa Walimu wenye Uwezo ........ 22
2.4 Ufundishaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika Lugha ........ 23
2. 5 Mapengo ya Utafiti ........ 24
2.6 Kiunzi cha Kinadharia ........ 25
2.7 Muhtasari ........ 26
METHODOLOJIA YA UTAFITI ........ 27
3.1 Utangulizi ........ 27
3.2 Paradima ya Utafiti ........ 27
3.3 Usanifu wa Utafiti ........ 27
3.4 Eneo la Utafiti ........ 28
3.5 Wango, Sampuli na Usampulishaji ........ 28
3.5.1 Wango ........ 29
3.5.2 Sampuli ........ 29
3.5.3 Usampulishaji ........ 29
3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa ........ 30
3.6.1 Data za Msingi ........ 30
3.6.2 Data za Upili ........ 30
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 31
3.6.1 Usomaji Matini ........ 31
3.6.2 Mahojiano ........ 31
3.7 Zana na Vifaa vya Utafiti ........ 31
3.8 Uchanganuzi wa data ........ 32
3.9 Itikeli ........ 33

3.10 Muhtasari....................................................................................33
SURA YA NNE: MJADALA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI....................................................................................34
4.1 Utangulizi....................................................................................34
4.2 Uelewa wa Walimu na Wakuu wa Masomo kuhusu Stadi ya Kusoma na Kuandika na MUU....................................................................................34
4.2.1 Hoja tofauti Kuhusu Dhana ya Stadi ya Kuandika....................................................................................35
4.2.2 Hoja tofauti kuhusu Dhana ya Kusoma....................................................................................36
4.2.3 Hoja tofauti kuhusu Dhana ya MUU....................................................................................37
4.3 Mbinu Zinazotumiwa na Walimu katika Ufundishaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika....................................................................................39
4.4 Changamoto Zinazokabili Walimu Wanapofundisha Stadi za Kusoma na Kuandika....................................................................................44
4.4.1 Ukosefu wa Utamaduni wa Kuandika na Kusoma....................................................................................45
4.4.2 Ukosefu wa Vifaa Vinavyohitajika katika Kusoma na Kuandika ...46
4.4.3 Ukosefu wa motisha miongoni mwa Wanafunzi....................................................................................47
4.4.4 Uhaba wa Walimu wenye Uwezo....................................................................................50
4.5 Mikakati Inayoweza Kutumiwa na Walimu katika Ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika....................................................................................51
4.5.1 Utumiaji wa TEHAMA....................................................................................52
4. 5.2 Utumiaji wa Andaa- Shiriki na Tafakari....................................................................................53
4.5.3 Utumiaji wa Usomaji na Uandikaji Gawizwa....................................................................................55
4.5.4 Utumiaji wa Ujenzi wa Maarifa....................................................................................57
4.6 Mchango wa MUU katika Ufundishaji wa Stadi Ya Kusoma na Kuandika 59
4.7 Muhtasari wa Sura ya Nne....................................................................................63
SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO....................................................................................64
5.1 Utangulizi....................................................................................64
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti....................................................................................64
5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza....................................................................................64

5.2.2 Lengo Mahususi la Pili ........................................................... 65
5.2.3 Lengo Mahususi la Tatu ........................................................... 66
5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika ........................................................... 66
5.4 Hitimisho ........................................................... 67
5.5 Mapendekezo ........................................................... 68
5.5.1 Mapendekezo kwa Walimu Wanaofundisha Kiswahili ........................................................... 68
5.5.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu pamoja na Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda ........................................................... 69
5.5.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ........................................................... 69
5.5 Muhtasari wa Sura ya Tano ........................................................... 70
MAREJELEO ........................................................... 71
1. Mwongozo wa Mahojiano kwa Walimu wa Kiswahili ........................................................... 76
3. Kibali cha Kukusaya Data ........................................................... 79

# ORODHA YA VIFUPISHO

**Dkt.:** Daktari

**Khj**: Keshatajwa hapo juu

**MUU**: Mtaala Unaoegemea katika Uwezo

**REB**: Bodi ya Elimu ya Msingi Rwanda

**TEHAMA**: Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**T.Y.**: Tafsiri yetu

**Whj**: Wameshatajwa hapo juu

# UTANGULIZI

## 1.0 UTANGULIZI

Sura ya kwanza inahusisha utangulizi wa ujumla wa tasnifu hii. Tasnifu hii ililenga kuchunguza namna ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za sekondari zilizopo nchini Rwanda. Sura hii inazingatia taarifa za awali zinazohusiana na utafiti wote kama vile usuli na tamko la tatizo la utafiti, malengo na maswali, umuhimu, mawanda na mpangilio wa utafiti pamoja na muhtasari wa sura husika.

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kwenye enzi za sasa, mabadiliko ya haraka na ya kina kwenye soko la ajira duniani kutokana na maendeleo ya teknolojia na utandawazi yameleta changamoto katika sekta ya elimu (Mutare na Malambo, 2019). Ili kukabiliana na changamoto hizi, wadau wa sekta ya elimu walifanya juu chini ili kutafuta mbinu zinazoweza kutumiwa ili kutayarisha wahitimu wa elimu ambao watafaulu kwenye soko la ajira. Katika harakati za uundaji wa mbinu hizo, stadi za kusoma na kuandika zilipendekezwa miongoni mwa stadi za msingi zinazohitaji kusisitiziwa katika mchakato wa elimu katika enzi za sasa ili kuandaa wahitimu wa elimu ambao wataweza kufaulu kwenye soko la ajira. Park na Kyei (2007) wanaeleza kwamba stadi za kusoma na kuandika ni stadi muhimu ambazo zinahitajika ili kufanikisha mwanafunzi kufaulu siyo tu kwa masomo bali pia katika maisha ya kila siku.

Kwa mjibu wa Haigler, Harlow, O’Connor & Campbell (1994), stadi za kusoma na kuandika ni uwezo alio nao binadamu ambao humwezesha kusoma na kuandika. Uwezo huu sio rahisi kama unavyosikika kwa kuwa unatofautiana

kutokana na tamaduni, miktadha na nyakati. Kusoma na kuandika ni zaidi ya kutambua na kuelewa maandishi. Kusoma na kuandika ni stadi ambazo zinaweza kuathiri utambuzi na ugunduzi miongoni mwa wanajamii (Dotson, Kitner-Triolo, Evans na Zonderman, 2009).

Stadi za kusoma na kuandika ni stadi muhumu sana hasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha (Zaiter, 2020). Katika mchakato wa kufundisha na kujifunza lugha ni bora mwanafunzi aanzie kwenye stadi ya kusoma na kuandika; stadi hizi zinakamilishana katika ujifunzaji na ufundishaji lugha. Hapa ni kusema kuwa, mtu hawezi kuboresha stadi moja na kuacha nyingine. Kuandika na kusoma hushughulikiwa pamoja. Kinachosomwa kiliandikwa mara ya kwanza au kutolewa kwa njia ya mdomo. Kilichoandikwa kinakusudiwa kusomwa. Mchakato wa kufundisha na kujifunza kusoma pamoja na kuandika huchukuliwa kama kitengo cha dhana na somo la kufundisha na kujifunza. Zaiter (Khj) anaendelea akieleza kwamba mtu asiyejua kusoma na kuandika hawezi kujifunza lugha kiurahisi na kama mtu hajui lugha yoyote ile, hawezi kukabiliana na changamoto za maisha ya enzi za sasa.

Hivyo basi, ili kuandaa wahitimu wa elimu ambao watakaoweza kufaulu kwenye soko la ajira, nchi kadhaa zilibadilisha mifumo ya kielimu zikaanza kutumia Mtaala Unaoegemea katika Uwezo ambao kuanzia sasa utarejelewa kama MUU katika utafiti wetu. MUU ni mtaala unaosisitiza kile wanafunzi wanachotarajiwa kufanya badala ya kuzingatia zaidi kile wanachotarajiwa kujua. Kwa mjibu wa Nzima (2016), msingi wa MUU ni nafasi ya wanafunzi katika kuleta maarifa, ujuzi, mitazamo na imani katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Harakati za ubadilishaji wa mtaala wa kielimu na kuanza kutumia MUU zilijitokeza kwenye nchi kadhaa. Marekani MUU ulianza kutumiwa mwaka wa 1970 (Kitta na Tilya, 2010), nchini Iran mwaka wa 1999 (Sotco na Mwandanji, 2015), nchini Zambia mwaka wa 2013 (Chisholn, 2007), nchini Cameroon

mwaka wa 2002 (Mbei, 2018), Tanzania mwaka wa 2005 (Likisa, 2018), nchini Rwanda mwaka wa 2015 (Likisa, Khj). MUU ulianza kutumiwa kwenye nchi kadhaa ili kuhusisha elimu inayotolewa na hali halisi ya maisha kwa kusaidia wanafunzi kupitia maarifa, ufahamu, stadi na maadili (Chisholn, Khj). MUU ulipoanza kutumiwa, ulilenga kukuza uwezo wa kimsingi katika uraia na utambulisho wa kitaifa, uzalishajimali na maendeleo ya kibiashara, TEHAMA, sayansi na tekinolojia, kuhesabu pamoja na kusoma na kuandika (Kabombwe & Mulenga, 201). Miongoni mwa stadi za msingi zinazosisitiziwa katika MUU, stadi za kusoma na kuandika huchukuliwa kama stadi muhimu ambazo zinashiriki sana katika ujifunzaji wa stadi nyingine.

Ni lazima mwanafunzi amudu vilivyo lugha inayotumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji ili aweze kufaulu (Park na Kyei, 2007). Hali hii inatokana na ukweli kwamba uwezo unapaswa kukuzwa kupitia lugha anayoielewa mwanafunzi kwani kila somo hufundishwa kupitia lugha. Kwa hiyo, ni bora kusisitizia stadi za kusoma, kuandika, kuongea na kusikiliza lugha ili kutimiza malengo ya kielimu.

Stadi za kusoma na kuandika zilisisitiziwa katika utekelezaji wa MUU kwa sababu zimedhihilishwa kama stadi muhimu katika ujifunzaji wa lugha. Mosi, Rosiana (2014) katika utafiti wake kuhusu ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika Kifiji katika muktadha wa mtaala mpya, alionesha kuwa stadi za kusoma na kuandika hufanikisha wanafunzi kuimudu lugha ya Kifiji inayotomiwa nchini Fiji. Pili, Sandra & Rod (2016) walifanya utafiti kuhusu stadi ya kusoma na kuandika katika ufundishaji Kifaransa kwa wanafunzi wanaojifunza katika shule za msingi teule nchini Ufaransa. Matokeo yaliyopatikana kwenye utafiti wao yalionesha kuwa kusoma na kuandika ni stadi muhimu sio tu katika ujifunzaji wa Kifaransa bali pia katika ujifunzaji wa masomo mengine. Isitoshe, Adamson (2014) alionesha kwamba stadi za kusoma na kuandika haziwezi kutenganishwa na ujifunzaji wa lugha yoyote ile.

Tafiti za watafiti wa hapo juu zinaonesha kuwa kusoma na kuandika ni stadi zinazohitaji kuendelezwa ili kuimarisha ujifunzaji wa lugha. Ingawaje, mambo mengi muhimu kuhusu stadi za kusoma pamoja na kuandika na ujifunzaji wa lugha, tafiti za hapo zina mapengo yalitusukuma mpaka tukaamua kufanya utafiti huu ili kuyaziba mapengo hayo. Mosi, tafiti za hapo juu zilijikita sana kwa wanafunzi wa shule za msingi, hakuna utafiti wowote uliogusia wanafunzi wa shule za sekondari. Pili, tafiti hizi zilishughulikia ujifunzaji wa lugha kupitia uimarishaji wa stadi za kusoma na kuandika bila kuhusisha MUU. Tatu, tafiti za watafiti wa hapo juu zinazungumzia nchi tofauti kama vile Malanezia, Ufaransa na Tanzania ambazo mazingira yake ni tofauti na mazingira ya Rwanda. Mwisho, hakuna utafiti hata mmoja uliofanywa kuhusu kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika kwa kujiegemeza kwenye MUU kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda.

Kwa hiyo, mapengo ya tafiti zilizotangulia, yameamsha kiu ya kitaaluma ya mtafiti kutaka kuchunguza hali ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi mbili ambazo ni kusoma na kuandika Kiswahili ilivyo kwenye nchi ya Rwanda. Kwa hivyo, utafiti wetu ulichunguza namna stadi za kusoma na kuandika zinavyoweza kufundishwa kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za upili wilayani Nyamagabe.

## 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Kama tunavyozidi kuingia kwenye karne ya ishirini na moja, ni lazima kufahamu hatua tunazoweza kuzipiga ili kuimarisha maendeleo endelevu ya wanajamii. pia, ni lazima kutambua kuwa lugha ni muhimu sana kwa elimu bora (Epçaçan, 2018). Kwa hiyo, ili wanafunzi wajue lugha vizuri, wanatakiwa kujua kusoma na kuandika lugha hiyo. Stadi za kusoma na kuandika ni stadi muhimu zinazohitajika ili kuandaa wahitimu wa elimu ambao wataweza kufaulu kwenye soko la ajira (Brock**,** 1990**;** Holmarsdottil, 2002 & Rugemalira, 2005).

Ingawaje tafiti zimeonesha kuwa kuandika na kusoma ni stadi sinazohitajika ili kufanikisha shughuli za kufundisha na kujifunza lugha na masomo mengine, ilibainika kuwa stadi za kusoma na kuandika kwa wanafunzi zingali kwa kiwango cha chini. Jambo hili huathiri sana ujifunzaji wa lugha (Dos Santos, 2008; Adamson, 2015 na Huul, Sempson, Guo & Wang, 2015). Zaidi ya hayo, kwa kadiri ya uelewa wetu, hakuna utafiti uliofanyika nchini Rwanda kuhusu mchakato wa kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Ukosefu wa tafiti kuhusu kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika katika MUU huathiri sana ufundishaji kwa kuwa huwanyima walimu na wadau wengine wa sekta ya elimu taarifa kuhusu namna ambavyo stadi za kusoma na kuandika huweza kuimarishwa ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Hivyo basi, utafiti wetu ulikuja kuchunguza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe.

### 1.3.1 Lengo la Jumla

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe nchini Rwanda.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti wetu yalikuwa:

i) Kubainisha namna ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe.
ii) Kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika utekelezaji wa MUU kwa shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe.

iii) Kubainisha mikakati inayoweza kutumiwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika kupitia MUU kwa wanafunzi wa shule za upili za wilaya ya Nyamagabe.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Tasnifu hii ilikusudia kujibu maswali matatu ambayo ni pamoja na:

i) Je, ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kwenye shule za upili kwenye wilaya ya Nyamagabe unafanyikaje?

ii) Je, ni changamoto zipi zinazokabili utekelezaji wa ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kwa shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe?

iii) Ni mikakati ipi inayoweza kutumiwa na walimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Nyamagabe?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti ulioibua tasnifu hii unahusu uchunguzaji wa ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma pamoja na kuandika katika MUU kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe nchini Rwanda.

Utafiti huu utakuwa na manufaa anuai kinadharia na kiutendaji. Mosi, matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuweka mipango mikubwa ya namna ya kutekeleza kwa ufanisi shughuli ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika MUU kwa wanafunzi wa sekondari na wengineo wanaojifunza stadi hizo.

Pili, Matokeo ya utafiti wetu yatawasidia walimu kuboresha mafundi yao ya ufundishaji ili kurahisisha utimizaji wa malengo kufundisha na kujifunza stadi ya kusoma pamoja na kuandika katika muktadha wa MUU kwa wanafunzi

wanaosoma katika shule za sekondari. Vilevile, matokeo ya kazi yangu ni rejeleo muhimu katika utungaji wa sera na watafiti wengine watakaofanya utafiti katika eneo linalowiana na utafiti huu. Hali kadhalika, utafiti huu utawasaidia wanafunzi kuimarisha stadi za kusoma na kuandika kwa kupitia MUU.

## 1.6 Mawanda ya Utafiti

Utafiti wetu ulikuwa mawanda yafuatayo:

### 1.6.1 Mawanda ya Kimaudhui

Japokuwa kuna stadi nyingi za lugha (kusoma, kuandika, kusikia na kuzungumza), utafiti huu ulijikita zaidi katika kufundisha na kujifunza stadi za kusoma pamoja na kuandika kwa kuzingatia utekelezaji wa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo. Tumeteua stadi za kusoma pamoja na kuandika kutokana na madai ya wataalamu kuwa stadi hizi zinaathiriana sana katika mchakato wa ujifunzaji. Pia, katika utafiti huu mtafiti ameamua kujikita katika usomaji na uandishi katika kujifunza na kufundisha lugha ya Kiswahili ikizingatiwa kuwa lugha hii huwatatiza wafundishaji na wajifunzaji wengi tofauti na Kinyarwanda au Kifaransa.

### 1.6.2 Mawanda ya Kijiografia

Kwa upande wa jiografia, utafiti wetu ulifanyika wilayani Nyamagabe katika Mkoa wa Kusini. Wilaya ya Nyamagabe imechaguliwa kwa kuwa tunaamini kuwa ilitusaidia kupata taarifa zote muhimu zilizotufaa kwa kutimiza malengo ya utafiti. Wilaya hii ina pia shule zenye mchepuo wa lugha zinazojifunza lugha ya Kiswahili kutoka kidato cha nne hadi cha sita.

### 1.6.3 Mawanda ya Kimuda

Kwa wakati, utafiti ulisisitizia kwenye kipindi cha wakati cha kati ya 2021 – 2022. Lengo kuu lilikuwa kuchunguza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za

kusoma na kuandika katika MUU kwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Nyamagabe kwenye nchi ya Rwanda.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti

Vikwazo vilivyokabili kazi ya utafiti hii na namna tulivyokabiliana navyo imeelezwa hapo chini:

a. Katika ukusanyaji wa data, kuna watoataarifa kama vile walimu na wakuu wa masomo waliojaribu kutupa taarifa ambazo si za kweli ili kuzipa shule zao sura nzuri.Ili kuepuka changamoto hii, watoataarifa wengi waliulizwa na majibu yao yakalinganishwa ili kupata uamuzi wa jumla.

b. Kutokana na kwamba idadi ya watu wanaojua lugha ya Kiswahili si wengi, haikuwa rahisi kwetu kupata taarifa zilizohitajika hasa hasa wakati wa usaili. Ili kuepuka kikwazo hiki, maswali yaliyoulizwa wasailiwa yalikuwa kwa lugha mbili, yaani Kiswahili na Kiingereza.

## 1.8 Mpangilio wa Utafiti

Tasnifu imegawanyika katika sura tano ambazo ni sura ya kwanza iliyotoa utangulizi wa jumla kuhusu utafiti, sura ya pili iliyozungumzia mapitio ya maandiko na nadharia ya utafiti, sura ya tatu iliyoangazia methodolojia ya utafiti, sura ya nne iliyohusiana na uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti na sura ya mwisho ambayo ilitoa muhtasari, hitimisho pamoja na mapendekezo mbalimbali.

## 1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura ya kwanza imeeleza sehemu za msingi katika utafiti wowote wa kitaaluma. Vipengele hivyo ni kama vile utangulizi, usuli na tamko la tatizo la utafiti, malengo, maswali, umuhimu, mawanda na mpangilio wa utafiti pamoja na muhtasari wa sura husika.  Sura ambayo inafuata inazungumzia mapitio ya maandiko na nadharia ya utafiti.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia maandiko mbalimbali yaliyopitiwa na kutumiwa kwenye kazi hii. Sura ya mapitio ya maandiko tumeigawa katika sehemu zifuatazo: Stadi ya kuandika, stadi ya kusoma, ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi ya kusoma na kuandika, mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma na kuandika, mbinu za kusoma na kuandika, mtaala unaoegemea katika uwezo na utekelezaji wa kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika katika MUU. Sura hii pia ina nadharia itakayotumika katika utafiti huu.

## 2.1 Dhana ya Stadi ya kuandika

Ujuzi wa kiisimu haujakamilika bila uwezo wa kutosha wa kuandika. Kuandika vizuri kunamaanisha kuweza kuwasilisha mawazo yako kwa ufupi. Sio lazima uandike sentensi ndefu, ngumu zilizojaa msamiati mgumu ili kuandika vizuri. Unachohitaji ni uwezo wa kuwasilisha mawazo yako kwa sentensi fupi ambazo zinaweza kutoa ujumbe kamili. Kuandika vizuri kunafaa sana kwa sababu ndiko kunakosaidia wanajamii katika shughuli zao za kila siku sikiwemo mawasiliano, biashara, uandishi wa barua, vitabu makala na mengineyo (Choo, 2010). Stadi ya kuandika ni uwezo maalumu ambao huwasaidia waandishi kuweka mawazo yao katika maneno kwa umbo lenye maana inayolingana na kile wanachokifikilia. Kwa hiyo, kuandika ni shughuli au mchakato wa kutoa wazo au maoni ya mtu fulani.

Zaidi ya hayo, Charmeux (2014) anaeleza kuwa kitenzi "kuandika" katika Kifaransa kina hasara ya kujumuisha maana mbili tofauti kabisa, lakini ambazo tofauti zake kwa muda mrefu zimefichwa na polisemia hii. Kwa upande mmoja, anataja shughuli ya ufafanuzi wa kiisimu wa lugha ya maandishi inayokusudiwa kuonekana kwenye maandishi ya kijamii (barua, makala, bango na kadhalika) na

ambayo inaweza kusemwa kuwa "shughuli ya kijamii na kisaikolojia". Na kwa upande mwingine, kitenzi hikihiki kinaashiria shughuli ya utambuzi wa nyenzo ya usaidizi unaokusudiwa kupokea maandishi haya ambayo ni dhahiri shughuli ya kisaikolojia. Kwa mtazamo huu, kitenzi cha kuandika kinarejelea vipimo viwili. Mosi, kuandika kwa maana ya "uzalishaji", yaani, kuzalisha aina ya maandishi (kwa kurejelea uchapaji wa maandishi), kwa hiyo ni sehemu ya mwelekeo wa mawasiliano.

Utayarishaji wa maandishi hurejelea, kwa upande mmoja, kuzingatia mchakato wa utambuzi wa mwandishi na, kwa upande mwingine, usimamizi wa lugha ya Kifaransa, kwa hivyo sifa iliyotolewa na Charmeux ya shughuli za "kijamii na kisaikolojia". Pili, kuandika kwa maana ya "mchoro" inafanana na shughuli ya kuunda barua, sentensi au maandishi. Hapa ni swala la kukuza maandishi yanayokubalika kiisimu, kama kitu cha nyenzo, kwa hivyo sifa ya mwandishi wa shughuli za kisaikolojia na utambuzi.

Kutokana na maelezo hapo juu, tunaona kuwa kuna njia kadhaa za kufafanua dhana ya "kuandika", neno linalojumuisha ukweli tofauti kulingana na utamaduni. Katika utafiti huu, kuandika kutachukuliwa kwa maana ya kwanza ya Charmeux (Khj) kama tulivyoeleza hapo juu.

Kwa upande wa Brown (2001), kuandika ni mchakato wa kufikiri. Unaohusisha ufahamu, akili timamu na juhudi, ambazo kwa kawaida lazima ziungwe mkono kwa muda mrefu. Zaidi ya hayo, uandishi unapaswa kutayarishwa na kufanyiwa masahihisho ya kutosha kabla ya kutolewa. Urquhart & McIver (2005) wanaeleza kuwa, kuandika ni mchakato unaojirudia, ambao una maana kwamba wanafunzi hufikiria tena kupitia mchakato huo mara kwa mara wakisonga mbele hatua kwa hatua. Kisha, wanafunzi wanapaswa kujifunza mbinu za uvumbuzi na ugunduzi, na walimu wanapaswa kuwasaidia wanafunzi kuzalisha maudhui na kugundua madhumuni. Kutokana na maelezo haya, ufafanuzi wa stadi ya kuandika

unaweza kupatikana. Kuandika ni mchakato zalishi unaofanywa kupitia hatua fulani. Kwanza, kuchunguza na kupeleka mawazo, hoja na hisia katika maandishi. Pili, kuongoza idadi ya marekebisho ya mchakato kwa utekelezaji wa sarufi na mpangilio wa matini. Mazao ya uandishi yanajitokeza katika miundo ya matini yanayosomwa na yanayopaswa kuwa na maana kwa kila mtu anayesoma maandishi. Zaidi ya hayo, kutokana na maelezo haya, ifahamike kuwa stadi ya kuandika ni shughuli ngumu katika uandishi bora (Kitchakarn, 2012). Ugumu wa kazi ya uandishi unaonekana hatua kwa hatua katika uandishi. Kutokana na ugumu wa stadi ya kuandika kama ilivyodokezwa na Kitchakarn (Khj), tumeona tuchunguze hali ilivyo kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe.

Uandishi umechukuliwa kama stadi muhimu sana katika kufundisha na kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili kwani ni stadi ya kina ambayo husaidia kuimarisha msamiati, sarufi, kufikiri, kupanga, kuhariri, kusahihisha na vipengele vingine. Kuandika pia husaidia kuboresha stadi zote za kusikiliza,kuzungumza na kusoma kama yote yanahusiana (Wambui, 2011). Kutokana na umuhimu wa stadi hii kama ulivyodokezwa na wataalamu hapo juu, ndiyo maana tumeamua kuchunguza stadi hii na kuacha stadi ya kusikiliza na kuzungumza.

Kuandika kunahusisha pande mbili ambazo ni aliyeandika na anayesoma. Msomaji huwa mbali na mwandishi ndio sababu lugha inayowekwa katika maandishi inapaswa kuwa rahisi ili anayesoma aweze kuelewa kila kitu kilichoandikwa ili asiwe na maswali ya kujiuliza kutokana na kilichoandikwa. Katika stadi ya kuandika, matumizi ya taratibu za uandishi pamoja na matumishi ya alama za vituo, herufi kubwa na aya huzingatiwa. Stadi ya kuandika ina ubora wa kuwezesha watu walio mbali kuwasiliana na kuwa na maelezo yaliyoandikwa na ya kudumu kwa kuwa hayawezi kufutika. Kwa kuwa mwandishi huzingatia

kwa makini kanuni za kisarufi ili msomaji wake aweze kuelewa vyema, hustawisha sarufi ya lugha na misingi yake (Harmer, 2004).

Kama tulivyoeleza hapo juu, stadi ya kuandika ni muhimu sana katika lugha na pia ni muhimu zaidi ukilinganisha na stadi nyingine za lugha. Kwa mujibu Harmer (Khj), kuna umuhimu mkubwa wa kujifunza kuandika. Kwanza, kama ilivyo kwa maandishi, wanafunzi mara nyingi huwa na wakati mwingi wa kufikiria kuliko wanavyofanya katika kazi za mazungumzo. Pili, wanaweza kupitia kile wanachokijua katika akili zao, na kutafuta kwenye kamusi, vitabu vya sarufi, au nyenzo nyingine za marejeleo za kuwasaidia kung'amua maana. Tatu, uandishi pia huwahimiza wanafunzi kuzingatia matumizi sahihi ya lugha na kwa sababu wanafikiri wanapoandika, huenda ukasababisha ukuzaji wa lugha wa kusuluhisha matatizo ya maandishi yaliyomo akilini mwao (Harmer, Khj).

Kulingana na maelezo ya hapo juu, inaweza kuhitimishwa kuwa ufafanuzi wa kuandika ni mchakato wa kuendeleza mawazo, kufikiri juu ya jinsi ya kueleza mawazo hayo na kuyapanga katika aya ambazo hutumika kuwasiliana na watu wengine kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kupitia stadi ya kuandika, mwanafunzi hupata fursa ya kuelezea yaliyomo akilini mwake.

Ingawaje, maelezo ya hapo juu ni mazuri sana, hayaelezi waziwazi hatua zinazoweza kufuatiliwa ili kuimarisha stadi za kuandika lugha za kiafrika mithiri ya Kiswahili kwa wanafunzi hasa wa shule za sekondari. Hivyo basi, utafiti wetu ulikusudia kuchunguza namna ambavyo stadi ya kuandika inaweza kuendelezwa katika muktadha wa MUU kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za upili za wilaya ya Nyamagabe. Isitoshe, utafiti wetu umedhihirisha hatua zinazoweza kufuatiliwa na waelimishaji hasa wa lugha katika uhamasishaji wa stadi ya kuandika kwa wanafunzi wa shule za upili.

## 2.2 Dhana ya Stadi ya Kusoma

Kusoma ni utaratibu wa kuelewa ujumbe mwandishi anaotarajia kufikisha kwa wasomaji kupitia maandishi yake. Ili msomaji aelewe andiko la aina yoyote ile, ni lazima atumie muda wake kuelewa dhamira ya awali ya mwandishi. Kusoma vizuri na kwa undani kunahitaji siyo tu umakini kamili bali pia ufanisi unaowezesha msomaji kufikiri zaidi ya sentensi iliyoandikwa kwa madhumuni ya kuelewa ujumbe uliotolewa (Alderson, 2000). Unaweza kutoa maelezo, kuongeza maoni au kufupisha yaliyomo kwenye maandishi ili kupata ufahamu wa kina.

Miricho na wenzake ( 2008), wakinukuliwa na Lichuma (2018), wanaeleza kuwa stadi ya kusoma inahusu ujuzi wa mwanafunzi wa kusoma maandishi kwa mtiririko bila kusitasita, kwa sauti inayosikika na matamshi sahihi ya Kiswahili. Hivi ni kusema kuwa, mwanafunzi anapaswa kutilia mkazo kwenye matamshi bora, kiimbo na shadda. Anatarajiwa pia kukielewa anachokisoma, kukifasiri na kuweza pia kukieleza kwa njia inayoeleweka. Kusoma kunamsadia mwanafunzi kupata maarifa, kuelewa namna ya kutumia kamusi na maktaba, kupanua msamiati wake na kustawisha mazoea ya kupenda na kufurahia kusoma matini mbalimbali. Kusoma kunamtayarisha mwanafunzi katika ufasiri wa maneno anayoyasoma na katika uelewaji wake.

Kwa upande mwingine Giasson (2003) anaeleza kuwa kusoma kunachukuliwa kuwa mchakato wa lugha unaohitaji mikakati ya kutabiri, uthibitisho na ushirikiano. Pia kunachukuliwa kuwa mchakato wa mawasiliano, mchakato amilifu na mwingiliano. Gérard na Braibant (2003) kwao kusoma ni uzalishaji wa maana unaofanywa na mtu binafsi kutoka kwenye maandishi yaliyoandikwa.

Chauveau (2010) anasisitiza umuhimu wa mwelekeo wa lugha na mwelekeo wa kitamaduni. Kuhusiana na mwelekeo wa lugha, anabainisha kuwa, kusoma ni kuchakata na kuelewa kauli, ujumbe wa maneno yanayowekwa katika maandishi

(sentensi au matini). Vipimo viwili muhimu vya usomaji ni kusimbua na kuelewa kwa kuzingatia vipengele vya kitamaduni. Ili mwanafunzi ajue kusoma, ni lazima azipate ili asome kwa ufahamu.

Maelezo ya hapo juu yanaonesha kwamba kusoma sio tu kusimbua na kubainisha maneno au mfuatano wa maneno bali pia ina kuchunguza, kuhoji, kuzalisha na kuunda upya uzalishaji wa lugha kama vile hadithi, ripoti ya tukio na kadhalika. Maelezo haya mazuri, yanaishia tu kueleza maana ya stadi ya kusoma. Hayaoneshi kinagaubaga mikakati inayoweza kutumiwa ili kukuza stadi za uandishi kwa wanafunzi wanaojifunza katika shule za sekondari. Kwa hiyo, tasnifu hii inakuja kuziba pengo hilo kwa kuwa utabainisha taratibu zinazoweza kuzingatia ili kukuza stadi ya kuandika kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyamagabe. Baada ya kuchunguza fasili zilizotolewa kuhusiana na dhana ya stadi ya kusoma, tulipitia maandiko kuhusu aina za usomaji mbinu pamoja na madhumuni ya kusoma.

### 2.2.1 Aina za usomaji

Patel na Praveen (2008) wamebainisha aina kadhaa za usomaji kama inavyoelezwa hapo chini.

Mosi, kuna usomaji kimya. Patel & Praveen (whj) wanaeleza kwamba usomaji kimya ni aina ya usomaji unaohusiana na kusoma bila sauti. Usomaji kimya unaruhusu msomaji kusoma bila kuoa sauti. Inamaanisha kwamba usomaji huu unaweza kuzihusisha sauti ndogondogo au hotuba kimya za ndani zinazofanywa msomaji anaposoma andiko fulani (Bojovic, 2008). Maelezo haya yanatuonesha kuwa usomaji kimya ni mchakato wa kiakili ambao hupunguza athari za kiutambuzi zinazoweza kumuathiri msomaji wakati wa kusoma. Kwa hiyo, usomaji huu unasaidia akili kupata maana kwa kuiwezesha kukumbuka na kuelewa kile kinachosomwa.

Pili, kuna usomaji kwa sauti ambao ni aina ya usomaji unaofaa wasomaji kusoma matini kwa kutoa sauti kubwa kwa ajili ya kufurahia na kukuza stadi ya kusoma. Ili kufanikisha usomaji huu, msomaji anaweza kupewa aina nyingi za maandishi ya kusoma kama vile vitabu, majarida, magazeti na mengineyo.

Dalaney (2008) anaeleza kuwa kadiri mwanafunzi anapozidi kusoma maandishi kadhaa kwa sauti, anaweza kufurahia anayoyasoma na kupata hamu ya kutaka kusoma mengi. Hii ni kumaanisha kwamba mwanafunzi anaposoma maandishi mengi, bila shaka, uwezo wake wa kusoma utasonga mbele.

Mwisho kuna usomaji kina. Aina hii ya usomaji inamfaa msomaji kwenda zaidi ya maneno yaliyotumiwa katika andiko kwa kujaribu kuhusisha kilichoandikwa na miktadha kadhaa ili kupata ujumbe kamili wa andiko zima (Bojovic, Khj). Usomaji kina ni aina ya usomaji unaozingatia nahau na msamiati na istilahi nyinginezo zilizotumiwa na mwandishi. Nahau na msamiati na istilahi hizo huweza kupatikana katika shairi, riwaya, matini, ripoti au drama. Kwa mfano, Wanafunzi kuzingatia maelezo ya kiisimu au kisemantiki ya usomaji na kuzingatia muundo wa maelezo kama vile sarufi, wanaweza kuelewa kila aina ya maandishi kupitia usomaji kwa kina.

Maelezo ya watafiti wa hapo juu yanaonesha wazi kuwa kuna aina tatu za usomaji ambazo ni pamoja na usomaji kimya, usomaji kwa sauti na usomaji kina. Maelezo muhimu yaliyotolewa hapo juu yana upunguvu kwa kuwa mosi, hayakueleza namna ambavyo aina hizo za usomaji zinaweza kufanikisha ujifunzaji wa stadi ya kusoma kwa ujumla.

Pili, hayakuonesha mikakati inayoweza kutumiwa ili kuimarisha aina hizo za usomaji miongoni mwa wanafunzi na mwisho, maelezo yaliyotolewa na watafiti wa hapo juu hayadhihirishi mchango wa aina hizo za usomaji katika kufundisha na kujifunza lugha. Hivyo basi, utafiti wetu umeliziba pengo hilio kwa kueleza

yote ambayo hayakuelezwa na tafiti zilizotangulia kwa kuonesha mikakati ya kufundishia aina za usomaji na kudhihirisha mchango wa aina za usomaji siyo tu kufundisha pamoja na kujifunza kusoma na kuandika bali pia katika kufundisha pamoja na kujifunza lugha kwa ujumla.

### 2.2.2 Mbinu za Kusoma

Kuna mbinu nyingi ambazo tunaweza kutumia ili kurahisisha usomaji wetu. Kwa mujibu wa Rahmad (2008), usomaji unaweza kusaidia zaidi sana ikiwa tunaweza kusoma vizuri. Mbinu kadhaa za usomaji zimeelezwa hapo chini.

Mbinu ya kwanza mwa hizo ni mbinu ya kuchanganua ambayo ni mbinu inayotumiwa mara nyingi unapotafuta neno kwenye simu au kamusi. Wakati huu unatafuta maneno muhimu au mawazo. Kuna hatua anuai za uchanganuzi kama vile kutaja taarifa mahususi unayotafuta, kuweka mabunio ya jibu na vidokezo vitakavyotumiwa kukusaidia kupata jibu. Kwa mfano, ikiwa ungekuwa unatafuta tarehe fulani, ungesoma aya hiyo haraka kwa kutafuta namba tu. Hatua nyingine ni kutumia vichwa na visaidizi vingine vyovyote ambavyo vitakusaidia kutambua ni sehemu zipi zinaweza kuwa na maelezo unayotafuta kwa kuchagua kusoma na kuruka sehemu za kifungu.

Mbinu ya pili ya kusoma ni kwa kuandika mawazo muhimu . Kuandika mawazo muhimu ni mbinu inayotumiwa kwa haraka ili kudondoa mawazo makuu ya maandishi. Hatua za kuandika mawazo ni kusoma kichwa cha habari, kusoma utangulizi au aya ya kwanza, kusoma sentensi ya kwanza ya kila aya nyingine, kusoma vichwa na vichwa vidogo, kusoma muhtasari au aya ya mwisho Rahmad (khj).

Maelezo haya yanaonesha kuwa mbinu ya usomaji ambayo huweza kutumiwa na msomaji ni kusoma andiko alilopewa kwa kuzingatia wazo muhimu kwa kila sehemu ya andiko. Utafiti huu umedhihirisha namna ambavyo kila mbinu ya

usomaji inaweza kuboreshwa na kutumiwa katika kufundisha na kujifunza stadi ya kusoma katika muktadha wa MUU kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za upili za wilaya ya Nyamagabe.

### 2.2.3 Madhumuni ya Kusoma

Kusoma ni shughuli yenye kusudi. Mtu anaweza kusoma ili kupata faida, habari au kuthibitisha maarifa yaliyopo. Mtu anaweza pia kusoma kwa furaha, au kuongeza ujuzi wa lugha inayosomwa. Kusoma pia kuna jukumu muhimu katika maisha ya raia. Kupitia kusoma, mtu anaendelea kufahamishwa juu ya mambo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ya nchi yake. Kusoma huathiri mitazamo, imani, viwango, maadili, maamuzi, na tabia zetu kwa ujumla. Pia, kusoma kunatengeneza fikra na matendo yetu. Madhumuni ya kusoma ni kuunganisha mawazo juu ya maandishi kwa yale ambayo tayari unajua. Msomaji lazima aelewe kuhusu somo ambalo alisoma ili kuunganisha mawazo.

Kwa mujibu wa William na Fredrika (2002), madhumuni ya kusoma ni pamoja na; kusoma kutafuta taarifa rahisi, kusoma ili kujifunza kutoka kwenye maandishi, kusoma ili kuunganisha habari, kusoma kuandika, kusoma ili kuhakiki matini na kusoma kwa ufahamu wa jumla. Kusoma kutafuta habari rahisi ni uwezo wa usomaji wa kawaida. Watafiti wengine wanaona kuwa ni mchakato huru wa utambuzi. Hutumika mara nyingi katika kusoma kazi ambazo ni bora zaidi. Kusoma kwa haraka kunahusisha, kwa asili, mchanganyiko wa mikakati muhimu ya kubahatisha ambapo inaweza kuwa katika maandishi, na kisha kutumia ujuzi wa msingi wa ufahamu wa kusoma kwenye sehemu hizo za maandishi mpaka wazo la jumla litengenezwe.

Kwa upande mwingine, kusoma ili kujifunza kutoka kwenye maandishi hutokea katika taaluma na mazingira ambayo mtu anahitaji kujifunza kiasi kikubwa cha habari kutoka kwenye maandishi. Aina hii ya usomaji inahitaji uwezo wa kukumbuka mawazo makuu, utambuzi na ujenzi tungo za balagha na

kuunganisha maandishi na msingi wa msomaji (Wambui, Khj). Vilevile kusoma ili kuunganisha habari kunahitaji uamuzi wa ziada kuhusu umuhimu wa jamaa wa kusaidiana ili kuunganisha habari zinazokinzana na uwezekano wa urekebishaji wa sura ya balagha kwa kupokea habari kutoka kwenye vyanzo vingi.

Aidha, kujua kusoma na kuandika na usomaji makini wa maandishi kunaweza kuwa vibadala vya kazi ya kusoma ili kuunganisha habari. Zote mbili zinahitaji uwezo wa kutunga, kuchagua, na kukosoa habari kutoka kwenye maandishi. Kusoma kwa ufahamu wa jumla hukamilishwa na msomaji mwenye ujuzi fasaha, kuunda uwakilishi wa maana ya jumla ya wazo kuu na uratibu mzuri wa michakato mingi chini ya kizuizi cha muda mfupi sana.

Kwa hiyo, madhumuni ya usomaji yanawahusu wanafunzi pamoja na watu wengine. Kwa hiyo, ni lazima mtu atakaye kumudu stadi ya kusoma azingatie madhumuni ya kusoma kwa kusoma maandishi mabalimbali ili kupata taarifa na maarifa ya kijamii anamoishi. Utafiti huu umechunguza namna ambavyo stadi ya kusoma inaweza kuimarishwa kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe ili kujivunia faida zitokanazo na kumudu stadi ya kusoma Kiswahili.

## 2.3 Changamoto Zinazokabili Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusona na Kuandika

Katika jamii kadhaa zilizoendelea katika utumiaji wa kiteknolojia, uimarishaji wa stadi ya kuandika na kusoma umemepewa kipau mbele na umechukua umuhimu mkubwa katika ufundishaji na ujifunzaji lugha. Hata hivyo jamii kadhaa za Afrika zikiwemo jamii ya Wanyarwanda, stadi za kusoma na kuandika ziko kwenye kiwango cha chini kwa ujumla (Malik na wenzake, 2014). Kiwango hiki cha chini kinasababishwa na changamoto kadhaa ambazo zinawakabili walimu wanapofundisha kusoma pamoja na kuandika.

### 2.3.1 Ukosefu wa Utamaduni wa Kusoma na Kuandika

Changamoto ambayo huwakabili walimu wanapofundisha kusoma na kuandika kwa shule za sekondari nchini Rwanda ni ukosefu wa utamaduni wa kusoma nchini Rwanda. Usomaji na uandikaji ni mojawapo ya stadi za ujifunzaji wa lugha kama inavyoelezwa na Samuelson & Warshauer (2010) wanaosema kwamba stadi za ujifunzaji wa lugha ni pamoja na ufahamu, usomaji, uandikaji na uzungumzaji. Katika stadi hizi nne zinazodokezwa na watafiti wa hapo juu, mbili baadhi ya hizo ambazo ni pamoja na na usomaji na uandikaji ni muhimu zaidi katika ufundishaji wa Lugha. Ruterana (2012) anaeleza kwamba kusoma na kuandika hutegemeana kwa kuwa usomaji ni kuangalia na kuelewa maana ya maandishi, maneno au alama zilizochapishwa; usomaji ni shughuli ya kipekee ya binadamu ambayo ina sifa ya tafsiri ya ishara au herufi katika maneno na sentensi zinazowasilisha habari na inayomaanisha kitu kwa msomaji.

Ruterana (Khj) anaendelea kueleza kwamba usomaji hukuza hamu ya msomaji ya kusoma akilenga kuelewa maana ya maandishi yaliyoandikwa na kuweza kutathmini umuhimu wake na namna anavyoweza kutumia kile alichokisoma ili kujiongezea ujuzi, ufanisi na raha.

Ingawaje utamaduni wa kusoma na kuandika kwa hiari ni muhimu siyo tu kwa matumizi ya kibinafsi na ujifunzaji wa muda mrefu hasahasa wa fasihi endelevu baali pia kwa ajili ya ukuzaji wa ubunifu miongoni mwa wanafunzi, utamaduni huu hukosekana kwa Wanyarwanda, jambo ambalo huwatatatiza waelimishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda hasa Wilayani Nyamagabe. Aidha, ukosefu wa utamaduni wa kusoma na kuandika hukumba maendeleo endelevu ya nchi ya Rwanda (Kerchner, 2000).

Kwa hiyo, utafiti wetu umekuja kuonesha namna ambavyo utamaduni wa kusoma na kuandika unaweza kuendelezwa miongoni mwa Wanyarwanda ili kufanikisha kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa shule za upili za wilaya Nyamagabe nchini Rwanda.

### 2.3.2 Ukosefu wa Vifaa Vinavyohitajika katika Kusoma na Kuandika

Kikwazo kinachokabili walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika kwa shule za upili nchini Rwanda kwa kiasi kikubwa ni uhaba wa vifaa vinavyohitajika katika kusoma na kuandika kwa watoto na watu wazima na uhaba wa maktaba zinazofaa nchini Rwanda(Ruterana, Khj). Uhaba na upatikanaji wa vifaa vinavyohitajika katika kusoma na kuandika nchini Rwanda ni changamoto nyingine ambayo inaathiri vibaya ufundishaji wa stadi ya kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za upili nchini Rwanda. Maktaba pekee zilizopo nchini Rwanda, ingawaje nazo hazina vifaa timamu, zinapatikana hasa katika vyuo vikuu. Kwa hiyo si rahisi kwa umma kwa ujumla kupata uwezo wa kujivunia matumizi ya vifaa hivyo vya usomaji. Kikwazo hiki kinapunguza maendeleo na mafanikio ya ufundishaji wa kusoma na kuandika nchini Rwanda.

Zaidi ya kuwepo kwa maktaba maskini katika shule za upili nchini Rwanda ambazo zina vifaa vichache vya usomaji, vitabu vichache vinavyopatikana katika maktaba hizo viko katika Kiingereza na Kifaransa. Ni vigumu sana kupata vitabu vya Kiswahili katika maktaba hizo. Walimu wa Kiswahili ambao wanahitaji vitabu vya kutosha vilivyoandikwa katika lugha ya Kiswahili husumbuka sana na hufeili kufanikisha shughuli za kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika Kiswahili.

Kutokana na athari kubwa ambazo ukosefu wa vifaa vya uandikaji na usomaji unaweza kuleta kwenye ufundishaji wa stadi ya kusoma na kuandika, tumeamua kuufanya utafiti huu ili kudhihirisha namna ambavyo athari hizo mbaya huweza

kuepukwa na walimu wanaofundisha Kiswahili katika shule za sekondari kwenye wilaya ya Nyamagabe.

### 2.3.3 Ukosefu wa motisha miongoni mwa Wanafunzi

Neno motisha linahusiana na maneno matatu ambayo ni nia, utashi na hiari. Motisha hufasiliwa kama mchakato wa usimamizi uliopangwa, ammbao unachochea watu kufanya kazi kwa ewezo wao, kwa kuwapa nia ambayo inategemea mahitaji yao yasiyotimizwa (Tremblay, 2002).

Mwalimu huru Gara (2018) anaripoti jinsi alivyowapa baadhi ya wanafunzi vitabu vya watoto alivyokuwa ameleta nchini Rwanda kutoka katika kijiji chake ili kuchunguza ikiwa wanafunzi wa Rwanda wana utashi na motisha ya kuandika na kusoma vitabu kadhaa, alishangazwa na kupata kwamba 80% ya wanafunzi waliopewa vitabu vya kusoma hawakusoma hata ukurasa mmoja wa vitabu walivyopewa. Hapa ndipo alipoamua kwamba ukosefu wa motisha ya kusoma miongoni mwa wanafunzi ni changamoto ambayo hukumba ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika nchini Rwanda kwa kuwa mtu asiyesoma hawezi kuandika vilivyo.

Kwa mjibu wa Gardener (2002) ingawaje mwalimu anapaswa daima kuwasilisha jambo kwa njia ambayo itawavutia wanafunzi, hii imekuwa changamoto kubwa hasa kwa walimu wengi kwa kuwa watoto wengi hawana utashi wa kujifunza. Jambo linalosababisha ukosefu wa motisha ya kujifunza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi ni imani patofu kuhusu lugha ya Kiswahili ya kuihusisha na watu wenye vitendo wanaotenda maovu wahuni, wezi, virukanjia na wezi. Imani hii ilianza kusambaa wakati wa ukoloni wa Wabelgiji nchini Rwanda waliopendelea Kifansa dhidi ya Kiswahili. Jambo hili linaweza kukumba walimu wanapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili kwa shule za sekondari nchini Rwanda kutokana na kwamba Kiswahili kilitazamwa kama lugha duni ambayo si lazima kujifunzwa kwa kina.

Utafiti wetu umekuja ili kuwaonesha walimu wanaofundisha Kiswahili kwenye shule za sekondari nchini Rwanda namna ambavyo wanaweza kuwamotisha wanafunzi na kuondoa imani hizo potofu kuhusu lugha ya Kiswahili ili kuhamasisha ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi ya kuandika na kusoma kwa kujiegemeza kwenye matakwa ya MUU.

### 2.3.4 Uhaba wa Walimu wenye Uwezo

Changamoto nyingine ambayo inaweza kukabili walimu wanapofundisha kusoma na kuandika ni uhaba wa walimu wenye uwezo. Kwa mujibu wa Jonson (2001), mwalimu mwenye uwezo ni mwalimu ambaye ana angalau sifa za kitaaluma zinazohitajika kwa ajili ya kufundisha masomo yake katika ngazi husika katika nchi fulani. Tatizo la uhaba wa walimu wenye uwezo lilitafitiwa na watafiti kadhaa. Watafiti hawa wanaeleza kwamba uhaba wa walimu wenye uwezo ni tatizo ambalo huathiri ufundishaji wa lugha tofauti katika nchi mbalimbali. Jonson (2001) anasema kwamba uhaba wa walimu wenye uwezo uliathiri ufundishaji wa stadi ya kusoma na kuandika Kiingereza katika shule za sekondari nchini Ukraine.

Fema (2003) anafafanua kwamba ukosefu wa walimu wenye uwezo ni mojawapo ya mambo yanayosababisha wanafunzi kufanya makosa ya kimaandinshi na kimaongezi katika lugha ya Kiingereza nchini Naijeria.

Tafiti za hapo juu zinaelezea sana uhusiano uliopo kati ya walimu wenye uwezo na ufundishaji wa Kiingereza. Hazielezi namna ambavyo uhaba wa walimu wenye uwezo huweza kuathiri ufundishaji wa stadi ya kusoma na kuandika lugha za kibantu kama vile Kiswahili ambazo ni tofauti kabisa na Kiingereza. Pengine, ingawaje, Kimenyi (2003) anasema kwamba uhaba wa walimu wenye uwezo huathiri ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda, haelezi namna ambavyo uhaba huo huathiri walimu wanapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili za nchi ya Rwanda katika muktadha

wa MUU. Utafiti huu unalenga kuziba mapengo yaliyodhihirika katika tafiti zilizotangulia.

## 2.4 Ufundishaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika Lugha

Kwa mujibu wa Braun (2004), kufundisha ni mwongozo na vifaa vya kujifunza, kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kuweka mazingira ya kujifunzia. Inamaanisha kwamba Kufundisha kusoma ni kuwasaidia wanafunzi kusoma lugha kwa ufasaha katika masomo yao darasani. Inahitaji kutumia aina ya istilahi kama vile mkabala, au mbinu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kufundisha hakuwezi kutenganishwa na kujifunza kwa sababu ufundishaji unaongoza na kurahisisha ujifunzaji, kuwezesha wanafunzi kujifunza na kusimamia hali ya kujifunza. Uelewa wa mwalimu wa jinsi wanafunzi wanavyojifunza utaamua falsafa yao ya elimu, mtindo wa kufundisha, mbinu na darasani (Braun, Khj). Kufundisha kunakuwa mwingiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Mchakato wa ufundishaji lazima uwe mzuri pale ambapo mwalimu anatakiwa kutumia mbinu mwafaka zinazotumika katika mchakato wa kielimu.

Kutokana na mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji uliodokezwa hapo juu, tumeamua kuchunguza jinsi unavyofanyika kwa wanafunzi wa darasa la nne wilayani Nyamagabe.

Kuhusu stadi za lugha, kusoma kuna jukumu muhimu. Kwa mfano, siku hizi, kuna magazeti mengi, na mitandao, tunaweza kupata baadhi ya makala za Kiswahili.

Ur (2009), anasema kwamba wakati mwingine tunapata maandishi rahisi zaidi kuelewa, hivyo ni vigumu kuhukumu, kwa kuwa kiwango chetu cha Kiingereza ni wazi pia lakini kwa kiongozi, pengine kusudi linaweza kuwa rahisi kwa sababu ya utayarishaji wa mada na msamiati ambao ulitolewa kupitia maswali yanayohusiana na maandishi. Imeelezwa hapo juu kuwa kusoma ni mchakato

mgumu, siyo kusoma tu maandishi lakini msomaji lazima aweze kuelewa ujumbe wa mwandishi ili msomaji aweze kueleza wazo lake, kukisia hitimisho ili kuhifadhi habari. Kuhusu umuhimu wa kusoma, mafundisho ya kusoma yanapaswa kuanza mapema iwezekanavyo.

Kusudi kuu katika ufundishaji wa kusoma ni kuwafanya wanafunzi kutumia maarifa yao ili kuwasaidia katika ufahamu wao wa kusoma maandishi. Kuongeza kasi, na kadhalika. Al katika Fahimsyah (2008), alisema kuwa kuna hatua za msingi za kufundisha kusoma kwa madhumuni ya kukuza ufahamu wa wanafunzi. Hatua hizo ni kuanzisha au kutengeneza maarifa ya usuli muhimu kwa kuelewa maandishi, kuweka nia ya kusoma (tambua maneno ya utafutaji ya swali la kujibiwa, utabiri uliothibitishwa), wanafunzi wasome kwa madhumuni haya, waambie wanafunzi jinsi ya kusoma kwa namna fulani (kwa kujibu swali, muhtasari, kusoma habari muhimu kwa sauti) kama wao wamekidhi malengo. Hatua ya mwisho, wape wanafunzi maoni kuhusu utendaji wao wa ufahamu. Vilevile, Kusimbua ni mbinu ya kumwezesha mtoto kutamka maneno ambayo ameyasikia hapo awali lakini bila kuyaona kimaandishi. Hatua hii ni muhimu katika mchakato huu kwa kuwa inaunda misingi mingine ya kusoma.

### 2. 5 Mapengo ya Utafiti

Kuna watafiti mbalimbali waliofanya utafiti kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika. Tafiti hizo zilionesha kuwa stadi za kusoma na kuandika ni stadi muhimu katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha kwa madhumuni ya kutatua tatizo la uhaba wa wafanyakazi wenye uwezo lililopo katika soko la ajira wanajamii (Chisholn, 2007; Park na Kyei, 2007; Dotson, Kitner-Triolo, Evans na Zonderman, 2009; Zaiter, 2020; Kitta na Tilya, 2010 & Sotco na Mwandanji, 2015).

Ingawaje tafiti hizi zinaeleza mambo mengi kuhusu stadi ya kusoma na kuandika pamoja na ujifunzaji wa lugha, tafiti hizi zina mapengo kadhaa ambayo yatazibwa

na utafiti huu. Mapengo hayo ni haya yafuatayo: Mosi, tafiti zilizofanywa hazikusisitizia ngazi ya elimu ambapo stadi ya kuandika na kusoma huweza kuimarishwa ili kutimiza malengo ya kielimu.

Pili, tafiti zilizotangulia utafiti wetu hazikudhihirisha waziwazi mbinu zinazoweza kutumiwa na walimu wa lugha ili kufundishia stadi za kusoma na kuandika miongoni mwa wanafunzi. Istoshe, tafiti za hapo juu zilihusu nchi zenye miktadha na mazingira tofauti na mazingira ya nchi ya Rwanda. Mwisho, hakuna utafiti hata mmojo uliofanywa kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma na kuandika katika MUU. Hivyo basi, utafiti wetu ulichunguza namna stadi za kusoma na kuandika zinavyotumiwa kufundisha na kujifunza lugha katika MUU kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe.

## 2.6 Kiunzi cha Kinadharia

Nadharia ni utaratibu, misingi pamoja na kanuni ambazo hujengwa kwenye namna ya mawazo kwa lengo la kutumiwa kama mwongozo wa kuelezea mambo fulani (Massamba, 2004). Kwa hiyo, utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Utamadunijamii. Mwasisi wa nadharia hii ni Vygotsky (1997). Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa mwingiliano wa jamii na taasisi zake kama vile shule au nyumba za ibada katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Nadharia hii imeteuliwa kwa sababu inadokeza umuhimu wa taasisi kama vile shule katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Nadharia hii ina mihimili miwili. Mhimili wa kwanza ni wa uunganishaji wa mawasiliano na shughuli za kijamii. Mhimili huu unasisitizwa kuwa, ili mtu aweze kujifunza lugha ya pili kwa ufanisi sharti mawasiliano yake yaunganishwe na shughuli mbalimbali za kijamii kama vile shughuli za kilimo, ufugaji, biashara, sherehe na mambo ya ibada. Mhimili huu ulitusaidia kukamilisha lengo la kwanza la tasnifu hii la kubainisha namna ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za upili kwenye wilaya ya Nyamagabe.

Mhimili wa pili ni wa uunganishaji wa nadharia na vitendo katika kujifunza lugha ili kukidhi haja ya mawasiliano. Mhimili huu unadokeza ujifunzaji wa lugha ya pili katika mazingira rasmi ambapo kunakuwa na miongozo rasmi inayowekwa katika utendaji ili kuona ufaafu wake. Mhimili huu ulitufaa sio tu kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika bali pia kuonesha namna ya kuboresha shughuli za kufundisha stadi za kusoma na kuandika kupitia MUU kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe.

### 2.7 Muhtasari

Katika sura ya pili, tulipitia maandiko ya watafiti wengine waliofanya utafiti kuhusu stadi za kusoma na kuandika pamoja na ujifunzaji wa lugha. Maandiko yaliyopitiwa yalitoa mwangaza wa kitaaluma kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kwa madhumuni ya kutimiza malengo ya kielimu. Bila shaka, utafiti wetu utakuwa muhimu kwa wanafunzi, walimu, wadau wa sekta ya elimu na watafiti wengine watakaotaka kufanya utafiti kuhusu kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojifunza katika shule za sekondari kwenye nchi ya Rwanda.

# METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura ya tatu tumejadili methodolojia ya utafiti inayohusisha mbinu mbalimbali za utafiti. Dawson (2002) anaeleza mbinu za utafiti kuwa ni kanuni za jumla au falsafa zinazomwongoza mtafiti kufanya utafiti wake. Kwa upande wao, Kombo & Tromp (2006), wanaeleza methodolojia ya utafiti kuwa ni utaratibu unaotumiwa na mtafiti wakati wa kufanya utafiti. Mbinu hizo huanzia kuteua eneo la utafiti mpaka uchanganuzi wa data zilizopatikana. Mbinu zinazorejelewa kwenye sehemu hii ni paradima, usanifu, eneo la utafiti, wango, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanyia data, zana na vifaa vya utafiti na mkabala wa uchanganuzi wa data. Pia masuala ya kiitikeli yamefafanuliwa katika sura hii.

## 3.2 Paradima ya Utafiti

Paradima ya utafiti ni kipengele muhimu kinachohusu vigezo, zana pamoja, matatizo yanayoweza kukabili utafiti na mbinu ambazo mtafiti anatumia ili kutimiza malengo ya utafiti (Neuman, 2009). Ili kutimiza malengo ya utafiti, mtafiti alikubali na akatathmini majibu yote na kila hoja ambayo ilitolewa na washiriki wa utafiti ambao ni walimu na wakuu wa masomo katika shule zilizoteuliwa katika wilaya ya Nyamagabe. Aidha, mtafiti alijaribu kutumia mbinu zilizofaa kukamilishana ili kuondoa matatizo yote yaliyoweza kuathiri utimizaji wa malengo ya utafiti ulioibua tasinifu hii.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti huelezwa kama kipengele kinachohitajika ili kutuonesha taswira ya ulivyofanyika tangu utafiti unapoanza mpaka unapomalizika. Usanifu wa utafiti unadhihirisha picha ya mbinu zilizotumiwa na mtafiti katika kukusanya, kuchambua, kuchanganua na kuwasilisha data (Kothari, 2008). Tasinifu hii

tumejaribu kuzitumia mbinu ya usanifu ya uchunguzi ambao ulikuwa wa kifani. Hii ni mbinu ya kuteua eneo fulani maalum litakalofanyiwa utafiti na kusaidia mtafiti kupata data muhimu zitakazoshiriki katika kutimiza malengo ya utafiti wetu. Utafiti wetu utakuwa utafiti wa kitaamuli.

Kwa hiyo, wakati wa ukusanyaji data, tulikusanya data za kitamuli kuhusu ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi ya kuandika na kusoma Kiswahili katika shule za upili kwenye wilaya ya Nyamagabe kwenye nchi ya Rwanda. Data zilizokusanywa zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia madondoo na maelezo.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Katika kazi ya utafiti, eneo la utafiti huonesha mahali kazi ya utafiti ilipofanyika ili kuzikusanya data za msingi au za pili zinazowezesha mtafiti kutimimiza malengo ya utafiti wake (Kothari, 2008). Katika utafiti wetu, eneo la utafiti lilikuwa ni uwandani na maktabani. Utafiti huu ulifanyika katika Nchi ya Rwanda, Mkoa wa Kusini, na Wilaya ya Nyamagabe. Nchi ya Rwanda iliteuliwa kwa sababu matumizi ya Kiswahili ni madogo ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika ya Mashariki kama vile Uganda, Kenya na Tanzania. Kwa upande wa maktabani, utafiti wetu tuliufanyia kwenye maktaba ya Chuo Kikuu cha Rwanda kwa sababu ilitusaidia kupata machapisho mbalimbali yanayohusiana na utafiti wetu.

### 3.5 Wango, Sampuli na Usampulishaji

Sehemu hii iniangazia sehemu tatu kwenye methodolojia ya utafiti. Vipengele hivyo ni wango, sampuli na usampulishaji. Sehemu hizi vimefafanuliwa kama ifuatavyo:

### 3.5.1 Wango

Kama inavyoelezwa na Kothari (2004), wango humaanisha jumla ya watu au vitu mbalimbali vilivyotumiwa na mtafiti ili kukamilisha malengo ya utafiti. Kwenye tasnifu hii, wango lilihusisha walimu wa Kiswahili na wakuu wa masomo katika shule tatu zitakazoteuliwa katika wilaya ya Nyamagabe. Vilevile wango lilihusisha nyaraka na miongozo mbalimbali ya serikali ya Rwanda kuhusu elimu.

### 3.5.2 Sampuli

Kwa mjibu wa Babbie (1992), sampuli inamaanisha idadi ndogo sana ya wango inayotumiwa na mtafiti anapokuzanya data zinazomfaa katika utimizaji wa malengo mahususi ya utafiti wake. Kwa upande wake Kothari (2004), anaeleza sampuli kuwa ni watoataarifa ambao wamechaguliwa kutoka kwenye kundi fulani. Sampuli kwenye utafiti hutarajiwa kuwakilisha vitafitiwa au watoataarifa katika wango.

Hivyo ni kusema kwamba, matokeo yanayopatika kutokana na sampuli iliyotumika kwenye utafiti huakisi matokeo ya wango wote kiasi kwamba sampuli nyingine ikitumika tofauti na ya awali matokeo yanatarajiwa kuwa yaleyale. Utafiti huu ulitumia sampuli ya watoataarifa kumi (10) ambao ni walimu watano (5) na wakuu wa masomo watano (5) kutoka kwenye Shule ya Mtakatifu Nicolas Cyanika, Shule ya Mtakatifu Kizito Gikongoro, Shule ya Sekondari ya Gasaka na GS Ngororero katika Wilaya ya Nyamagabe. Vilevile kulikuwa na sampuli ya waraka wa serikali wenye sera ya elimu inayoeleza MUU.

### 3.5.3 Usampulishaji

Usampulishaji ni zoezi la kuteua idadi ndogo kwenye wango inayotumika katika utafiti. Kwa mujibu wa Kombo & Tromp (2006) usampulishaji huchukuliwa kama zoezi la kuchagua kundi  dogo linalowakilisha kundi kubwa ambapo matokeo yanayopatikana kutokana na sampuli iliyochaguliwa yanatakiwa kuwakilisha kundi zima. Mchakato huu unaweza kutumia mbinu nasibu, ambapo

vitafitiwa vyote vina nafasi sawa ya kuingia kwenye sampuli. Kwenye kazi yetu, tuliamua kutumia mbinu za usampulishaji ambazo ni usampulishaji nasibu sahili. Usampulishaji lengwa ulitumika kuwapata watoataarifa kumi (10) ambao ni wakuu wa masomo watano (5) na walimu wa Kiswahili (5). Vilevile, usampulishaji lengwa ulitumika kupata waraka wa serikali wenye sera ya elimu inayoeleza mtaala unaoegemea katika ujuzi.

### 3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa

Tulipokuwa tunatusanya data, tulijaribu kukusanya aina za data ambazo tuliziona kuwa zilitufaa zaidi katika utimizaji wa malengo mahususi ya utafiti wetu. Kwa hiyo, tulikusanya data za aina mbili ambazo ni data za msingi na za upili.

#### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi huhusisha data za asili zinazokusanywa na mtafiti fulani na ambazo hazijawahi kukusanywa, kuchambuliwa au kuwasilishwa na mtafiti yeyote kwenye tafiti zilizotangulia utafiti unaofanyika (Furlong, 1984). Data hizi za msingi zinaweza pia kuitwa data ghafi kwa kuwa huwa zinafanyiwa kazi kwa mara ya kwanza tu. Hivyo basi, kwenye tasnifu hii tulikusanya data za msingi kwa kuchanganua nyaraka za walimu na majibu yaliyotolewa na wasiliwa.

#### 3.6.2 Data za Upili

Data za upili huhusisha data ambazo tayari huwa zimekusanywa na kuwasilishwa katika tafiti zilizokusanywa (Yin, 1994). Data hizi zinakusanywa ili ziungane mkono na data za msingi ili kutimiza malengo ya utafiti. Data za upili hukusanywa kwenye vitabu, magazeti, majarida, tasnifu, Makala na nyaraka nyingine zinazoweza kupatikana kwenye wavuti na tovuti. Data za upili katika utafiti wetu, zilikuzanywa kutoka kwenye tovuti na maktaba za Chuo Kikuu cha Rwanda na shule za sekondari zilizoteuliwa wilayani Nyamagabe.

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji wa data humaanisha mbinu anazozitimia mtafiti kwenye ukusanyaji wa data zitakazomfaa katika utafiti wake (Kombo & Tromp, 2006). Kwenye tasnifu hii, mtafiti alitumia usomaji makini na uhojaji. Mbinu za usomaji matini na mahojiano zilikamilishana ili kukusanya data zilizotusaidia kukidhi malengo mahususi yaliyobainishwa.

#### 3.6.1 Usomaji Matini

Mbinu hii huhusisha usomaji wa nyaraka mbalimbali zilizohifadhiwa maktabani ili kupata data za utafiti. Katika mbinu hii mtafiti alisoma waraka wa serikali wenye sera ya elimu inayoeleza mtaala unaoegemea katika uwezo. Vilevile, katika mbinu hii mtafiti alirejelea matini mbalimbali zinazohusiana na shughuli za kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika kwa madarasa ya awali. Mbinu hii inalenga kupata data zitazotumika kufikia lengo mahususi la kwanza linalohitajia kubainisha namna kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika ilivyo katika shule za upili katika wilaya ya Nyamagabe.

#### 3.6.2 Mahojiano

Mahojiano ni mbinu inayohusisha kujieleza kwa mdomo katika kuuliza na kujibu maswali. Kwa mjibu wa Enon(1998) anaeleza kuwa ni mbinu ya kuuliza maswali ya ana kwa ana,  simu au barua pepe kati ya wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu swali la utafiti lililoainishwa. Mbinu hii iliteuliwa kwa sababu watoataarifa waliolengwa walikuwa wanapatikana kwa urahisi. Mahojiano haya yanaundwa na maswali yaliyopangwa na kutayarishwa kabla ya mahojiano, na baadhi ya maswali hutolewa na mtafiti moja kwa moja.

### 3.7 Zana na Vifaa vya Utafiti

Kombo & Tromp, (whj). Wanasema kuwa vifaa vya utafiti ni zana zote zilizotumika katika mchakato mzima wa kuchambua data zilizokusanywa tangu

unapoanza mpaka anapomaliza kazi ya utafiti husika. Katika kazi hii ya utafiti, mtafiti alitumia mahojiano kama zana ya kukusanyia data za utafiti uwandani. Mahojiano yalitumika kukusanya data za maandishi kuhusu changamoto zinazowakabili walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika na mapendekezo ya namna ya kuboresha mbinu zinazotumiwa na walimu wanapofundisha kusoma na kuandika kupitia Kiswahili MUU kwa wanafunzi wa darasa la nne.

Ili kukamilisha zoezi la kukusanya data kwa ufanisi na kuzihifadhi, zana hiyo ya utafiti ilitumika pamoja na vifaa vingine kama vile kompyuta, simu na madaftari ya kutunzia kumbukumbu, kalamu na faili. Faili lilitumika kutunzia kumbukumbu mbalimbali kwenye mchakato wa utafiti. Maswali ya mwongozo katika mahojiano yalitumiwa katika utafiti huu. Kwa upande wa kompyuta pakatwa ilitumika wakati wote wa utafiti kuanzia kuandaa pendekezo mpaka kuandika ripoti ya utafiti ulioibua tasnifu hii.

### 3.8 Uchanganuzi wa data

Uchanganuzi wa data huhusisha uchambuzi wa data zilizokusanywa, uainishaji na upangaji wa data kwenye makundi husika ili kukamilisha malengo ya utafiti. Data za utafiti katika tasnifu hii zilichanganuliwa kwa mkabala wa kitaamuli. Kwa mujibu wa Cohen, Manion na Morrison (2007), mkabala wa kitaamuli huhusisha maelezo zaidi wakati wa kuchanganua data kuliko takwimu. Mkabala huu umeteuliwa kwa sababu utafiti husika haunuii kuchunguza takwimu bali hali ya ufundishaji ilivyo na kupendekeza namna ya kuuboresha.

Uchanganuzi wote wa data uliongozwa na mihimili ya nadharia ya Utamadunijamii ya Vgotsky (1997) inayosisitiza uunganishaji wa nadharia na vitendo katika kujifunza lugha ili kukidhi mawasiliano. Kwa hiyo data zilizokusanywa kupitia usomaji matini pamoja na mahojiano zilichanganuliwa

kwa kutumia mkabala wa kitaamuli kwa kuongozwa na msingi wa nadharia ya utamadunijamii ili kufikia malengo mahususi ya utafiti wetu.

### 3.9 Itikeli

Utafiti wowote wa kitaaluma ni muhimu uzingatie itikeli ili matokeo yake yawe halisi na ya kuaminika. Kwa kuzingatia hoja hiyo, katika utafiti huu, mtafiti alizingatia itikeli mbalimbali za utafiti za Chuo Kikuu cha Rwanda kama ifuatavyo. Mosi, mtafiti alihakikisha amepata kibali kutoka kwenye uongozi wa Chuo Kikuu Cha Rwanda kabla ya kwenda kukusanya data uwandani. Pili, mtafiti alihakikisha kutowashawishi watoataarifa kwa fedha au kitu chochote ili watoe taarifa. Tatu, mtafiti alitunza siri za watoataarifa alizozibaini wakati wa kukusanya data hasa siri zinazohusu maisha binafsi ya mtoataarifa. Nne na mwisho, mtafiti aliepuka ubwakuzi wa kitaaluma katika mchakato wote wa utafiti. Hivyo popote kwenye utafiti huu ambapo wazo la mtu lilitumika, basi mtafiti alihakikisha anataja chanzo (anamrejelea mwandishi) ili kutojimilikisha wazo la mtu.

### 3.10 Muhtasari

Sura hii ilisisitizia methodolojia na mbinu zilizotumiwa wakati wa ukusanyaji wa data zilizotusaidia kutimiza malengo ya utafiti. Sura hii inazingatia vipengele vifuatavyo paradima, usanifu, eneo la utafiti, wango, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za ukusanyaji wa data, zana na vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data pamoja na itikeli.

# SURA YA NNE: MJADALA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Utafiti ulioibua tasnifu hii ulilenga kutimiza lengo kuu ambalo lilikuwa ni kuchunguza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika MUU kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za sekondari katika wilaya Nyamagabe nchini Rwanda. Utafiti wetu ulilenga kutimiza malengo mahususi ambayo ni pamoja na: kubainisha namna ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari wilayani Nyamagabe, kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa kusoma na kuandika katika utekelezaji wa MUU kwa shule za sekondari wilayani Nyamagabe na kupendekeza namna ya kuboresha ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kupitia MUU kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za sekondari wilayani Nyamagabe.

Kwenye sura hii, utafiti wetu ilizungumzia uwasilishaji pamoja na mjadala wa matokeo ya utafiti uliofanyika. Kwa hiyo, utafiti wetu utaangazia mambo yafuatayo: uelewa wa walimu kuhusu lugha, stadi za kusoma pamoja na kuandika na MUU, mbinu ambazo walimu huzitumia wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili, changamoto zinazokabili walimu wanapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili, mikakati inayoweza kutumiwa na walimu ili kuepuka changamoto zinazokabili walimu wanapofundisha stadi za kusoma pamoja na kuandika na mchango wa MUU katika kufundisha na kujifunza stadi ya kusoma pamoja na kuandika.

## 4.2 Uelewa wa Walimu na Wakuu wa Masomo kuhusu Stadi ya Kusoma na Kuandika na MUU

Ili kutimiza lengo mahususi la kubainisha namna ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari za wilaya

ya Nyamagabe, utafiti huu ulikusanya data kuhusu uelewa wa walimu kuhusu dhana ya lugha, stadi za kusoma na kuandika pamoja na MUU. Data hizi zilikusanywa kwa kuwa uelewa wa walimu na wakuu wa masomo kuhusu dhana za hapo juu unaweza kuathiri vizuri au vibaya mchakato wa kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili.

### 4.2.1 Hoja tofauti Kuhusu Dhana ya Stadi ya Kuandika

Stadi ya kuandika imeoneshwa na tafiti tofauti kama stadi muhimu katika ujifunzaji wa lugha yoyote ile.

> Language writing skills have nowadays an important social as well as educational function and its status has social prestige that is very high in the society. Therefore, teachers should know what does language writing skills require (Urbanova and Oakland, 2002: 31)
> Stadi ya kuandika lugha ina umuhimu mkubwa siyo tu kwa jamii bali pia kwa sekta ya elimu na hadhi yake inapewa kipau mbele katika jamii. Kwa hiyo, waelimishaji wanapaswa kujua stadi ya kuandika lugha inahusu nini (T.Y.).

Dondoo la hapo juu linasisitizia umuhimu wa stadi ya kusoma katika ufundishaji, ujifunzaji na katika jamii. Pia, linaonesha kuwa walimu wanalazimika kuwa na uelewa kuhusu stadi ya kusoma. Jambo hili lilituchochea kutaka kuchunguza uelewa wa wahojiwa kuhusu stadi ya kusoma. Ili kupata taarifa zilizotufaa, tuliuliza swali “Ni nini maana ya stadi ya kusoma?” Wasailiwa walijibu yafuatayo:

> Ina maana ya ujuzi wa kuunda maneno muhimu, na kuyapanga kisanaa ili yawe na ujumbe kamili. Tena, mojawapo wa stadi nne za lugha. Stadi hii inamwezesha anayesoma lugha kuiandika sawa ili aweze na kuisoma ifaavyo (Mwalimu 1).

Dondoo hili linaonesha kuwa mwalimu huyu anachukuwa stadi ya kusoma kama mojawapo ya stadi nne za lugha inayowezesha mtu kuandika na kusoma lugha kwa kumpa uwezo wa kisanaa wa kuunda na kupanga maneno kwa ajili ya kutoa ujumbe fulani. Jibu lililotolewa na mwalimu wa hapo juu lina dosari kwa kuwa mosi, jibu alilotoa linachanganya stadi ya kuandika na stadi ya kusoma. Pili, jibu lililitolewa linachanganya uandikaji wa lugha na uundaji na upangaji wa istilahi katika lugha. Tatu, inaonekana kuwa jibu lililotolewa linachangwa stadi ya kuandika na fasihi kwa kusema kuwa stadi ya kuandika ni uwezo wa kisanaa wa utumiaji wa lugha. Aidha, jibu lililotolewa linaenda kinyume na maana iliyotolewa na Choo (2010) aelezaye kuwa stadi ya kuandika ni uwezo maalumu ambao huwasaidia waandishi kuweka mawazo yao katika maneno kwa umbo lenye maana inayolingana na kile wanachokifikiria.

### 4.2.2 Hoja tofauti kuhusu Dhana ya Kusoma

Kuandika kunahusisha pande mbili ambazo ni mwandishi na msomaji. Kwa hivyo, baada ya kupata taarifa kuhusu dhana ya stadi ya kuandika tulitaka kutathmini uelewa wa walimu kuhusu dhana ya stadi ya kusoma.Ili kukusanya taarifa kuhusu uelewa wa walimu kuhusu dhana stadi ya kusoma tuliuliza swali “Ni nini maana ya stadi ya kusoma?” Data tulizopata ni hizi:

> Reading skills mean the act of taking part and going through a given document and look at the written material, understanding the given message (Mwalimu 3).
>
> Stadi ya kusoma inamaanisha kitendo cha kushiriki na kupitia hati fulani pamoja na kuangalia nyenzo zilizoandikwa na kuelewa ujumbe uliotolewa (T.Y.).

Dondoo hili linaonyesha kuwa stadi ya kusoma ni mchakato wa kushughulikia maandishi kwa madhumuni ya kufahamu ujumbe uliotolewa na mwandishi.

Baada ya kupata jibu la hapo juu tulimuuliza mwalimu mwingine ili tuwe na taarifa za kutosha kuhusu swali lililoulizwa. Mwalimu mwingine alijibu yafuatayo:

> Stadi ya kusoma lugha ni ile inayoenda sambamba na stadi kuandika. Katika lugha stadi ya kuandika ni muhimu sana kwani humwelekeza anayesoma lugha kulingana na matamshi na tahajia bora katika lugha kama tunavyojua kwamba lugha ni chombo cha kupashana habari (Mwalimu 4).

Kwa mjibu wa Mwalimu 4 stadi ya kusoma ni stadi inayoendana na uandikaji ambayo hufundisha matamshi na tahajia. Jibu lililotolewa na Mwalimu 3 lina dosari kwa kuwa anahusisha usomaji na utambuzi wa ujumbe bila kuhusisha matamshi na tahajia. Kwa upande mwingine, Mwalimu 4 anaonesha kuwa stadi ya kusoma inalenga matamshi na tahajia bora, akasahau kuhusisha mchango wa akili katika utambuzi wa ujumbe uliotolewa Janette (2007) ambaye hufafanua stadi ya kusoma kama uingiliano tata kati ya maandishi, msomaji na madhumuni ya kusoma, ambayo yameundwa kutegemeana na maarifa ya awali, uzoefu na ujuzi wa msomaji kuhusu kulingana na jamii na utamaduni wake.

### 4.2.3 Hoja tofauti kuhusu Dhana ya MUU

Madhumuni ya utafiti wetu yalikuwa kuchunguza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe. Hivyo basi, katika ukusanyaji data tuliuliza walimu na wakuu wa masomo maana ya MUU katika shule teule kwa kutumia swali hili "Ni nini maana ya Mtaala Unaoegemea katika Uwezo?" Wahojiwa walijibu:

> Mtaala unaogemea katika uwezo ni mpangilio wa mambo yatakayofundishwa katika kiwango cha masomo fulani tangu shule ya msingi kuendelea mpaka kwenye chuo kikuu

> na ambao humpa mtu ujuzi na maarifa ya kumwezesha kutumia katika nyanja tofauti za maarifa na hivyo kuweza kukabiliana au kupambana na maisha kwa ujumla (Mwalimu 4).

Dondoo hili linaonyesha kuwa MUU ni mtaala ambao unaonyesha ya kufundishwa shuleni ili kutoa ujuzi utakaowezesha mwanafunzi kukabiliana na changamoto za maisha.Baada ya kuona kuwa walimu hawakufanikiwa kueleza MUU vilivyo, tulikusanya taarifa kwa wakuu wa masomo kwa kutumia swali lilelile. Mkuu wa masomo katika shule moja alisema:

> MUU ni mtaala unaompa mwanafunzi nafasi ya kukuza ujuzi wa kujenga kipaji na kukuza kipaji na kiwango cha ujuzi katika usomaji wake. Na Mtaala huu unamfanya mwalimu kuwa mwelekezaji wa wanafunzi yaani, mtaala huu unamfasili mwanafunzi kutekeleza matendo katika usomaji wake badala ya kuweka kichwani tu yale yaliyosomwa na mwalimu (Mkuu wa Masomo 1).

Dondoo la hapo juu linaonesha ya kwamba mhojiwa husika anaufafanua MUU kama mtaala unaolenga kupanua ujuzi wa mwanafunzi na kipaji chake kwa kumshirikisha katika mchakato wa kielimu.

Maelezo yaliyotolewa na wahojiwa yanaonesha kuwa hawaelewi vilivyo maana ya MUU kwa kuwa maelezo waliyoyatoa yanaonesha kuwa MUU hulenga kukuza ujuzi tu, wakasahau ya kwamba MUU ni mtaala ambao hulenga kukuza ujuzi, stadi, maadili na mwenendo mwema ili kuandaa wahitimu wa elimu ambao wataweza kufaulu kwenye soko la ajira. Ukweli huu unaendana na maelezo ya Barman na Konwar (2011). Barman & Konwar (Whj) wanasema kuwa MUU ni mtaala unaolenga kukuza maarifa, ujuzi, ubunifu na maadili kwa kuendeleza stadi

ya utatuzi wa matatizo, mawasiliano, utafiti, ugunduzi, ubunifu, ushirikiano pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu miongoni mwa wanafunzi.

Sehemu hii imeonesha kuwa walimu hawana uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya lugha, stadi ya kusoma na kuandika pamoja na MUU na hili huweza kuathiri vizuri au vibaya ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika muktadha wa MUU kwa wanafunzi wa wa shule za sekondari. Sehemu inayofuata sehemu hii ni matokeo ya utafiti kuhusu namna ambavyo walimu hufundisha stadi za kusoma na kuandika.

### 4.3 Mbinu Zinazotumiwa na Walimu katika Ufundishaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika

Lengo lililokuwa la kwanza kwenye utifiti huu ni kubainisha namna ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari kwenye wilaya ya Nyamagabe. Ili kutimiza lengo hili tulichunguza namna ambavyo walimu wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe hufundisha sta za kusoma na kuandika. Tulikusanya taarifa kwa kutumia swali lifuatalo "Ni mbinu gani unazozitumia unapofundisha stadi ya kuandika kwa wanafunzi wako?". Mwalimu mmoja baadhi ya waliooulizwa alijibu yafuatayo:

> Ninafundisha stadi za kusoma na kuandika kupitia usomaji kimyakimya, kushirikisha wanafunzi katika mazoezi ya kuandika mmoja baada ya mwingine na kusoma kwa pamoja (Mwalimu 4).

Dondoo hili linaonesha kuwa mwalimu huyu anapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili, anawashirikisha wanafunzi kwa usomaji binafsi na usomaji kwa makundi. Mwalimu huyu hakudhihirisha wazi hatua anazozifuatilia ili afanikishe ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili. Mwalimu mwingine aliyeulizwa, alijibu haya:

> Ninapofundisha stadi za kusoma pamoja na kuandika kwa wanafunzi wangu, huwa

> ninawasomea kisha, nikawaomba kuandika ninayoyasoma kisha, nikawapa alama kulingana na wanayoyaandika (Mwalimu 5)

Dondoo hili linaonesha kuwa Mwalimu 5 anafundisha usomaji na uandikaji wa lugha ya Kiswahili kupitia tathmini ambapo wanafunzi hulazimika kuandika yanayosomwa na mwalimu kwa ajili ya kupata alama. Mbinu hii inayotumiwa na Mwalimu 5 inaonekana kuwa ina upungufu. Mosi, mbinu hii inasisitizia stadi ya kuandika kwa kusahau stadi ya kusoma. Pili, mbinu hii si shirikishi kwa wanafunzi hawapewi nafasi ya kusoma kutokana na kwamba ni mwalimu ambaye anawasomea.

Mwisho, mbinu hii si mbinu nzuri ya ufundishaji na ujifunzaji na inaweza kutumiwa zaidi katika kutathmini ikiwa malengo ya kufundishia na kujifunzia yametimizwa.

Zaidi ya hayo, wakati wa ukusanyaji data kuhusu mbinu ambazo walimu huzitumia wanapofundisha kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili hatukusahau kukusanya data kutoka kwa wakuu wa mosomo wa shule teule. Mkuu wa masomo mmoja alijibu yafuatayo:

> In this school while teachers are teaching reading and writing skills, they use dictation, project planning, summary making, answering by essay writing, model reading by teaches and individual student reading time (Mkuu wa Masomo 1).
>
> Katika shule hii wakati walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika, hutumia usomaji kwa wanafunzi, upangaji wa mradi, uandishi wa muhtasari, kujibu kwa uandishi wa insha, usomaji kielelezo unaofanywa na mwalimu na usomaji binafsi wa mwanafunzi (T.Y.).

Dondoo hili linaonesha kuwa walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika, wanatumia mazoezi ya uandikaji na kusomea wanafunzi kisha wakaiga

namna ambavyo mwalimu wao anasoma. Mbinu hii inaonekana kuwa haiwahusishi wanafunzi kwa kuwa haiwapi wanafunzi nafasi ya kushiriki katika ukuzaji wa uwezo wao wa kugundua namna bora ya kuandika na kusoma baadhi ya maneno yanayotumiwa katika lugha. Aidha, mbinu hii haendani na maelezo ya Brow (2001) anayesema kwamba ili kufanikisha shughuli za kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika, walimu wanalazimika kutumia mbinu ambazo huwezesha wanafunzi kukuza uvumbuzi na ugunduzi wa maudhui na madhumuni ya wanayoyaandika na wanayoyasoma.

Isitoshe, andalio la somo ni  kifaa bora katika kuboresha shughuli za kufundisha na kujifunza somo lolote lile kwa sababu andalio la somo huwapa walimu wasaa wa kupanga mbinu za kufundishia ili kukidhi mahitaji ya kujifunza kwa wanafunzi kwa urahisi (Oser & Baeriswl, 2001). Kwa hiyo, wakati wa ukusanyaji data kuhusu namna ambavyo walimu hufundisha sdadi ya kusoma na kuandika Kiswahili wilayani Kicukiro, tulichunguza maandalio ya masomo mbayo hutumiwa na walimu kwa kudadisi ikiwa kwa ukweli yanasisitizia uimarishaji wa kusoma na kuandika Kiswahili. Hapo chini mi mfano mmoja baadhi ya maandalio tofauti tuliyoyatathmini.

| Muhula: | Tarehe: | Somo: | Kidato: | Mada: | Somo la: | Muda: | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| wa kwanza | 10/11/2021 | Kiswahili | 4 LLK | 1 | 7 katika 45 | Dakika: 80 | 45 |

| | |
|---|---|
| Aina ya wanafunzi wenye mahitaji ya kielimu watakaoshughulukiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao | 0 |
| Mada | **LUGHA YA KISWAHILI** |
| Uwezo uhitajiwao katika somo | Kusikiliza , kuzungumza na kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano |
| Somo lenyewe | **ALFABETI KATIKA KISWAHILI** |
| Malengo ya kujifunza | Kwa kutumia vifungu mbalimbali, kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:<br>-Kuonesha kwa usahihi matumizi sahihi ya sauti za Kiswahili katika maandishi<br>-Kutumia msamiati wa Kiswahili kwa tahajia bora<br>-Kufurahia matumizi ya Kiswahili shuleni nan je ya shule |
| Mahali mbapo somo litafundishiwa | Somo litafundishiwa darasani |
| Vifaa au zana kwa wanafunzi wote | Kitabu cha mwalimu, kitabu cha mwanafunzi na kamusi |
| Vitabu vya rejelea | REB (2018). Kitabu cha Kiswahili IV, Kitabu cha Mwanafunzi & Mwalimu, Kigali. |

| Muda na hatua | Mbinu za kufundisia na kujifunzia | | Tafakuri tunduizi na maswala mtambuka vielezwe +maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| | Kwa kutumia vifungu vya habari tofauti, mwalimu atawawezesha wanafunzi kuhusisha mila na desturi mbalimbali katika kuaga na kumbulishana salamu, kuonesha kwa usahihi matumizi sahihi ya sauti za Kiswahili na kutumia msamiati husika kwa matamshi na tahajia bora kwa usahihi | | |
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| Utangulizi Dakika. 20 | Kuuliza maswali ya kukumbusha somo la awali | Kujibu maswali maswali ya kukumbusha somo la awali | Mawasiliano katika lugha rasmi.<br>(Kupitia njia ya kujadiliana na kujibu maswali ya mwalimu katika makundi, wanafunzi watumie lugha rasmi ya Kiswahili)<br><br>Tafakuri tunduizi: (wanafunzi kwa kutafuta maana ya matumizi ya kiambishi chenye dhana ya masharti)<br><br>Ujifunzaji wa muda mrefu |
| Somo lenyewe<br><br>Dakika: 50 | Kutoa tathmini tanguluzi<br><br>Kuwakaza wanafunzi kwenye makundi na kuwapatia wanavunzi tathmini endelezi<br><br>Kuchunguza ikiwa kazi wanafanywa na kutoa msaada kama unahitajika<br><br>Kuomba wanafunzi kwasilisha na kuwasaidia kusahihisha yaliyowasilishwa na kuyafanyia ufupisho | Kujibu maswali ya tathmini tangulizi<br><br>Kukaa kwenye makundi na kujibu maswali ya tathmini endelezi<br><br>Kufanya kazi na kuomba msaada kwa mwalimu kama unahitajika<br><br>Kuwasilisha, kuungana mkono na mwalimu katika kusahihisha yaliyowasilishwa, kuyafanyia ufupisho na kuuandika madaftarini | |
| Hitimisho Dakika: 10. | Kuoa tathmini jumuishi | Kujibu maswali tathmini jumuishi | |
| Tathmini ya mwalimu | Somo limefundishwa vizuri. | | |

**Kielelezo: Mfano wa Andalio la Somo (Data za Msingi, 2022)**

Kielezo hiki kinaonesha kuwa andalio la somo la hapo juu linahitaji kuboreshwa kwa kuondoa baadhi ya dosari zilizodhihirika. Mosi, kwenye sehemu ya "Uwezo Unaopatika katika Mada" kumeandikwa "Kusikiliza, kuzungumza na kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano". Sehemu hii ina kasoro kutokana na kuwa haihusishi stadi kasoma. Ili kuboresha sehemu hii, aliyeandaa andalio la hapo huu angeandika "kusikiliza, kuzungumza, kuandika na kusoma kwa madhumuni ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano". Pili, kwa upande wa "Malengo ya Kufundishia na Kujifunzia kunahitaji marekebisho kwa kuwa aliyeandaa somo la hapo juu hakugusia stadi stadi ya kusoma. Malengo yangeandikwa ifuatavyo:

“Kwa kutumia msamiati, tungo na vifungu vya habari mbalimbali katika lugha ya Kiswahili, mwishoni mwa somo hili kila mwanafunzi ataweza: i) Kuonesha kwa ufasaha matumizi ya fonimu za Kiswahili katika matamshi na maandishi, ii) Kutumia msamiati wa Kiswahili kwa matamshi na tahajia bora na iii) kujivunia faida zitokanazo na kuweza kusoma na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili. Isitoshe, mbinu za kufundishia na kujifunzia zinafaa kurekebishwa na kuandikwa ifuatavyo: “kwa kutumia misamiati, tungo na vifungu vya habari mbalimbali vya lugha ya Kiswahili, mwalimu atawaelekeza wanafunzi kukuza stadi za kuandika na kusoma kwa kuwaoa nafasi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili waweze kukuza ugunduzi na uvumbuzi wa namna bora ya kuandika na kusoma lugha ya Kiswahili.

Aidha, kutokana na data tulizokusanya wakati wa ukusanyaji data, tuliona kwamba walimu wa Kiswahili hawasisitizii ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili kutokana na kutoandaa masomo vilivyo na hii huathiri vibaya mafanikio kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika Kiswahili. Ukweli huu inathibitishwa na dondoo la hapo chini.

> Lack of planning skills among teachers affects negatively teaching and learning activities. Therefore, when teachers are not able to prepare teaching and learning materials, they can’t achieve educational objectives easily. This is why teachers are called upon acquiring lesson preparation skills that can help them to improve education quality (Letcja, 2015: 560).
>
> Ukosefu wa ujuzi wa kuandaa masomo huathiri vibaya kazi ya ufundishaji na ujifunzaji. Kwa hiyo, kama waalimu hawana uwezo wa kuandaa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, hawawezi kutimiza malengo ya kielimu kwa urahisi. Ndio sababu waalimu wanahitaji kukuza uwezo wao wa maandalizi

ya msomo ambao utawawezesha kuboresha elimu (T.Y.).

Dondoo la hapo juu linaonesha kuwa ukosefu wa uwezo wa kuandaa masomo miongoni mwa walimu huathiri vibaya ufundishaji na ujifunzaji na kuwachochea walimu kutumia mbinu hafifu ambazo haziwezi kuzaa matunda katika sekta ya elimu.

Kama tumemaliza kuonesha namna ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari kwenye wilaya ya Nyamagabe, sehemu inayofuta inaeleza changamoto za utekelezaji wa kufundisha na kujifunza stadi za kusoma pamoja na kuandika kwenye shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe.

## 4.4 Changamoto Zinazokabili Walimu Wanapofundisha Stadi za Kusoma na Kuandika

Ufundisha na ujifunzaji wa kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili ni jambo muhimu siyo tu kwa wanyarwanda bali pia kwa raia wote wa Jumuia ya Afrika Mashariki. Lengo la pili la utafiti wetu lilikuwa Kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa kusoma na kuandika katika utekelezaji wa MUU kwa shule za sekondari wilayani Nyamagabe. Ili kutimiza lengo hili kwanza, tuliongozwa na mhimili wa kwanza wa nadhalia ya utamatunijamii unaohusu uunganishaji wa nadharia na vitendo katika kujifunza lugha ya pili na mhimili wa pili wa nadhari hii usemao kuwa, ili mtu aweze kujifunza lugha ya pili kwa ufanisi sharti mawasiliano yake yaunganishwe na shughuli mbalimbali za kijamii kama vile shughuli za kilimo, ufugaji, biashara, sherehe na mambo ya ibada. Pili, tulipitia matini zinazohusiana na lengo la pili la utafiti wetu na mwisho tulitumia mahojiano kati ya mtafiti na walimu na wakuu wa masomo ili kutimiza lengo husika. Changamoto zilizobainishwa ni hizo hapo chini

### 4.4.1 Ukosefu wa Utamaduni wa Kuandika na Kusoma

Changamoto ya kwanza ambayo ilidhihirishwa miongoni mwa changamoto zinazokabili walimu wa shule za sekondari wilayani nyamagabe wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika ni ukosefu wa utamaduni wa kuandika na kusoma miongoni mwa wanafunzi katika madarasa ya lugha. Badamasi (2007) anasema kuwa utamaduni wa kuandika na kusoma huendelea mtu anaposoma maandiko mengi kuhusu mada tofauti ili kukuza uwezo wake wa kusoma na kuandika. Ingawaje utamaduni wa kusoma na kuandika huhitajika wakati wa kufundisha na kujifunza lugha, taarifa tulizopata wakati wa ukusanyaji data zinaonesha kwamba Wanyarwanda wanakosa utamaduni huu na hii huathiri vibaya kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika kwenye shule za upili za wilaya ya Nyamagabe hasa kwa madarasa ya lugha. Ukweli huu unadhihirishwa na dondoo la hapo chiniNyaraka tulizopitia zilionesha yafuatayo:

> One of the effects that affect language teaching and learning is that reading and writing culture among Rwandans is considered low with few people willing to take time to read and write (Nkurunziza, 2010: 4).
>
> Mojawapo ya athari zinazoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ni kwamba utamaduni wa kusoma na kuandika kwa Wanyarwanda ungali kwenye kiwango cha chini na watu wachache walio na hiari ya kuchukua muda wa kusoma na kuandika (T.Y.).

Dondoo hili linaonesha kuwa kiwango cha chini cha utamaduni wa kusoma na kuandika kwa Wanyarwanda kinaathiri walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za sekondari nchini Rwanda.

Zaidi ya hayo, wahojiwa sita (6) sawa na asilimi sitini (60%) kati ya wahojiwa kumi (10) walioshiriki katika utafiti wetu, kwa kujibu swali “Ni changamoto zipi unazokabiliana nazo unapofundisha stadi ya kuandika?”, walijibu kuwa ukosefu

wa utamaduni wa kusoma na kuandika ni mojawapo ya changamoto ambazo huwakabili wanapofundisha kuandika na kusoma Kiswahili kama inavyooneshwa na dondoo la hapo chini.

> Baadhi ya wanafunzi hawapendi kusoma na kuandika. Unapowapatia kazi inayowabidi kusoma na kuandika, unaona kwamba wanashindwa kutokana na kukiuka uakifishaji, sharia za kisarufi na uteuzi wa msamiati. Hili hujitokeza kwa sababu wanafunzi hawana uzoefu katika kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili (Mwalimu 5).

Hii ni kumaanisha kwamba walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika, huwa wanakabiliwa na changamoto inayotokana na uzoefu finyu wa kusoma na kuandika unaojidhihirisha miongoni mwa wanafunzi. Hoja hii haiendi kinyume na maoni ya Kerchner (Khj) anayeeleza kwamba ukosefu wa utamaduni wa kusoma na kuandika hukumba ufundishaji na ujifunzaji lugha nchini Rwanda.

### 4.4.2 Ukosefu wa Vifaa Vinavyohitajika katika Kusoma na Kuandika

Moja kati ya malalamiko yaliyoenea kwa muda mrefu kutoka kwa walimu wa Kiswahili chini Rwanda ni uhaba wa viafaa vya kufundishia kusoma na kuandika Kiswahili (Ruterana, 2012). Hivyo basi, uhaba wa vifaa vya kusoma na kuandika umedhihirishwa kama changamoto ambayo huwakabili walimu wa shule za sekondari wanapofundisha kuandika na kusoma Kiswahili katika utekelezaji wa MUU katika shule za sekondari wilayani Nyamagabe. Hoja hii huthibitishwa na majibu yaliyotolewa na wasailiwa wakati wa ukusanyaji data. Mmoja alisema:

> Kama mwalimu mwalimu wa Kiswahili, changamoto ambayo inanikabili ninapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili ni ukosefu wa vitabu vya Kiswahili na vifaa vingine kama kompyuta na zana nyingine zinazoweza kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma na kuandika Kiswahili (Mwalimu 5).

Mwalimu 5 anafichua kuwa anapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili anakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vifaa vya kusoma na kuiandika na hii huzuia wanafunzi kuzimudu stadi za lugha kusoma na kuandika. Dondoo la hapo juu linaendana na dondoo la hapo chini.

> Most children do not have access to books outside of school with only five per cent of children having access to books at home. Only six per cent of children have access to a library or somewhere in their community where they can read or borrow books." (Nkurunziza, 2012:4).
>
> Idadi kubwa ya watoto haina uwezo wa kupata vitabu vya hadithi nje ya shule kwa asilimia tano (5%) tu ya watoto ambao wanaweza kupata vitabu vya kusoma nyumbani kwao. Ni asilimia sita (6%) tu ya wanafunzi ambao wanabahatika kupata vitabu wanavyohitaji maktabani au mahali pengine ambapo wanaweza kuwaazimu vitabu (T.Y.).

Dondoo hili linaonesha kwamba nchini Rwanda wanafunzi hawana vifaaavya kusoma na kuandika vinavyoweza kuwasidia wanapojifunza kuandika na kusoma. Changamoto hii hukabili walimu hasa wale wanaofundisha katika shule za sekondari wilayani Nyamagabe kutokana na kwamba mazingira wanamofundishia huwanyima wanafunzi bahati ya kujifunza wapendavyo. Maelezo haya yanaendana na mhimili wa nadharia ya utamadunijamii unaosema kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili unahitaji mazingira rasmi ambapo kunakuwa na vifaa na miongozo rasmi inayowekwa katika utendaji ili kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.

### 4.4.3 Ukosefu wa motisha miongoni mwa Wanafunzi

Motisha inahitajika sana katika mchakato wa kufundisha na kujifunza lugha ya pili. Lennastson (2008) anafafanua kwamba motisha na nia ya kujifunza lugha ya

pili ni mambo yanayoweza kuathiri mchakato wa kufundisha na kujifunza lugha. Hivyo basi, matokeo ya utafiti wetu yameonesha kuwa changamoto ambayo hukabili mchakato wa kufundisha na kujifunza stadi za kuandika na kusoma ni ukosefu wa motisha kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za upili katika madarasa ya lugha wilayani Nyamagabe kwenye nchi ya Rwanda. Wahojiwa kwa kujibu swali "Kama mwalimu wa Kiswahili, ni changamoto zipi unazokabiliana nazo unapofundisha stadi ya kuandika na kusoma?" mmoja kati yao alisema:

> Kama mwalimu wa Kiswahili, changamoto nyingine inayonisumbua ninapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili ni utashi wa hali ya chini wa wanafunzi wa kujifunza lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wangu wanapenga Kingereza sana na hawapendi Kiswahili. Kwa hiyo, uwezo wao wa kusoma na kuandika Kiswahili ungali kwenye kiwango cha chini (Mwalimu 7).

Dondoo hili linaonesha kwamba baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe hawapendi lugha ya Kiswahili, jambo ambalo huzuia mafanikio wakati wa ujifunzaji na ufundishaji wa stadi sa kusoma na kuandika Kiswahili.

Aidha, wakuu wa masomo nao walidokeza kuwa ukosefu wa motisha kwa wanafunzi kunakabili walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili. Wakuu wa masomo kwa kujibu swali "Kama mkuu wa masomo, dhihirisha changamoto zinazokabili walimu wanapofundisha stadi ya kuandika na kusoma?", mmoja kati yao alijibu:

> One of the challenge that affects teach teachers when they are teaching Kiswahili reading and writing skills is the lack of motivation among students. Sincery speaking, students are not motivated to learn Kiswahili because they consider it as a language that

> will not be useful in their future live (Mkuu wa Masomo 4).
>
> Changamoto moja inayowaathiri walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili ni ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi. Kwa ukweli, wanafunzi hawahamasikii kujifunza Kiswahili kwa sababu wanaiona kama lugha ambayo haitakuwa na manufaa katika maisha yao ya siku zijazo (T.Y.).

Dondoo la hapo juu linaonesha kwamba ukosefu wa motisha kwa wanafunzi unakabili ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili kwa wanafunzi wa shule ya upili kwenye wilaya ya Nyamagabe kwa kuwa wanafunzi wanaipuuza lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti wetu yanalinga na matokeo ya utafiti wa Nasser & Majid (2011: 995) kama inavyooneshwa hapo chini.

> If language learners feel that mastering a language can’t be useful in the future, they will not enhance their motivation and will not do their best to achieve this goal within a short time (Nasser & Majid 2011: 995).
>
> Ikiwa wajifunzaji wa lugha hawaoni kuwa kumudu stadi za lugha hakuna manuafaa katika siku zijazo, hawatazidisha motisha yao na hawatafanya kila liwezekanalo kwa kutimiza malengo ya kujifunzia kwa muda mfupi (T.Y.).

Dondoo hili nalo linosisitiza kuwa kuidharau lugha kuna athari mbaya katika ufundishaji na ujifunzaji wa wa stadi za lugha. Kwa hiyo, ni ukweli usiopingika kuwa ukosefu wa motisha kwa wanafunzi unazuia walimu kufundisha vilivyo stadi za kusoma na kuandika Kiswahili kwa wanafunzi wa shule ya upili kwenye wilaya ya Nyamagabe.

### 4.4.4 Uhaba wa Walimu wenye Uwezo

Uwezo wa walimu unahitajika sana mchakato wa kufundisha na kujifunza stadi za lugha. Matokeo ya utafiti wetu yameonesha kuwa uhaba wa walimu wenye uwezo ni changamoto ambayo inaathiri ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili. Ukweli huu unathibithishwa na maelezo ya hapo chini yaliyotolewa na mkuu wa masomo mmoja.

> The challenge that hinder teaching and learning Kiswahili reading and writing skills is the lack of qualified Kiswahili teachers. When we have adapted the combination of languages we requested the district to provide our school with one teacher of Kiswahili. But unfortunately, because periods of Kiswahili can't be enough to complete the teacher's workload, the district refused to give us Kiswahili teacher. To fill this gap, we asked the teacher of English to help us to teach Kiswahili even though this teacher is not qualified in teaching Kiswahili. This affects our students' mastery of Kiswahili language (Mkuu wa Masomo 3).
>
> Changamoto inayokabili walimu wanapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili ni ukosefu wa walimu wa Kiswahili wenye uwezo. Tulipoanzisha mchepuo wa lugha, tuliomba wilaya kuajiri mwalimu mmoja wa Kiswahili kwenye shule yetu. Lakini kwa bahati mbaya, kwa sababu vipindi vya Kiswahili haviwezi kutosha kukamilisha ratiba kozi ya mwalimu, wilaya ilikataa kutupatia mwalimu wa Kiswahili. Ili kuziba pengo hili, tulimuomba mwalimu wa Kiingereza atusaidie kufundisha Kiswahili hata kama mwalimu huyu hakusemea kufundisha Kiswahili. Hii inaathiri umahiri wa wanafunzi wetu katika lugha ya Kiswahili (T.Y.).

Dondoo hili linaonesha kuwa walimu ambao hawana uwezo wa kutosha katika kufundisha kiswahili wanatumiwa kwa kuziba ufa wa uhaba wa walimu wenye uwezo wa kufundisha Kiswahili.

Uhaba huu huzuia mafanikio ya ufundishaji pamoja na ujifunzaji kusoma na kuandika Kiswali kwenye shule za sekondari wilaya ni Nyamagabe. Kimenyi (2003) anasema kwamba ukosefu wa walimu wenye uwezo huathiri ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa Kiswahili hasa kwenye shule za upili nchini Rwanda.

Kwa kuwa sehemu hii imedhihirisha changamoto zinazokabili uimarishaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili, katika seheme inayofuata tumejaribu kuonesha mikakati inayoweza kutumiwa ili kuepuka changamoto wanazokabiliana nazo wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za sekondari zilizopo kwenye wilaya ya Nyamagabe.

## 4.5 Mikakati Inayoweza Kutumiwa na Walimu katika Ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika

Baada ya kuona kuwa walimu wanakabiliwa na changamoto tofauti wakati wanapofundisha kusoma na kuandika, kwenye tasnifu hii tumeamua kupendekeza mikakakati inayoweza kutumiwa na walimu wa shule za sekondari ili kuimarisha mchakato wa kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili katika madara ya lugha. Tumefanya hilo kwa kujiegemeza siyo tu kwenye mahitaji ya MUU bali pia kwenye mhimili wa kwanza wa nadharia ya utamadunijamii usemao kwamba ili mtu aweze kujifunza lugha ya pili kwa ufanisi ni sharti ujifunzaji wake uunganishwe na shughuli mbalimbali za kijamii kama vile shughuli za kilimo, ufugaji, biashara, sherehe na mambo ya pili pamoja na mhimili wa pili na nadharia husika unaounganisha nadharia na matendo wakati wa kufundisha. Ifuatayo ni mikakati tuliyoiunda.

### 4.5.1 Utumiaji wa TEHAMA

Katika enzi za sasa ambapo dunia anazidi kuendelea katika uchumi, utandawazi na teknolojia, ni lazima waelimishaji hasa wa lugha ya pili waanze kutumia TEHAMA ambayo ni mbinu mpya ya kufundishia na kujifunzia ambayo ina mchango mkubwa katika utimizaji wa malengo ya kielimu (Pearson, 2003).

Kwa kutumia mbinu ya TEHAMA, mwalimu anaweza kuweka wanafunzi kuwaweka kwenye maabara ya kompyuta ambamo kuna mtandao wa intaneti. Kisha, mwalimu anaweza kuomba wanafunzi kukaa kwenye majozi na kufuata mwongozo wa usomamaji na uandikaji kwa tahajia bora ulioandaliwa na mwalimu.

Baadaye, mwalimu anaweza kuomba wanafunzi katika majozi yao kujaribu kuiga mfano wa usomaji na uandikaji wa vifungu vya Kiswahili walivyovifuata kwenye Kompyuta zao. Hapa, ili stadi za kusoma na kuandika ziimarishwe, ni lazima kila mwanafunzi apewe nafasi ya kushiriki katika usomaji na uandikaji.

Aidha, mwalimu anaweza kuomba mwanafunzi katika kila jozi kutunga kifungu kuhusu maisha ya kawaida kwa kufuata na kusanifu mfano aliopewa. Baada ya kutunnga kifungu hiki ni lazima kila mwanafunzi achangie na mwenzake aliyoyaandika na kujaribu kuyarekebisha wakiongonza na mwongozo waliopata kupitia TEHAMA. Bila shaka, kwa kufuata mwongozo huu, walimu wanaweza wakaboresha ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kuandika na kusoma Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Hii huthibitishwa na dondoo la hapo chini.

> ICT is very beneficial in terms of attracting students' attention. Students will be more interested in the lesson when we use ICT. They are more attentive in class and sometimes even a double-period is not enough. In fact, ICT tools are beneficial because they meet the teacher's teaching objectives (Melor, Norazah, Hadi, Choo & Mohamed, 2013).

> TEHAMA ina faida katika kuwamotisha wanafunzi. Wanafunzi wanavutiwa zaidi na somo tunapotumia TEHAMA katika ufundishaji. Wanafunzi wanavutiwa zaidi na mazingira ya darasa n ahata muda wa vipindi viwili hauwezi kutosha. Kwa hiyo, TEHAMA ina faida kwa kuwa inashiriki katika kutimiza malengo ya kufundishia (T.Y.).

Hii ina maana kwamba utumiaji wa TEHAMA unaleta hamu ya kufurahia kujifunza miongoni mwa wanafunzi kwa kulifanya darasa liwe pahali pazuri pa kujifunzia na pasipochosha wanafunzi. Maelezo haya huendana na mlimili wa nadharia ya utamadunijamii ya Vygotsky (1997) unaosisitizia umuhimu wa mwingiliano ujifunzaji, mazingira na jamii katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Mbinu hii ya utumiaji wa TEHAMA ni muhimu sana kwa kuwa inaweza kushiriki katika kutatua channgamoto ya ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi ambayo huwakabili walimu wanapofundisha kusona na kuandika Kiswahili.

### 4. 5.2 Utumiaji wa Andaa- Shiriki na Tafakari

Mbinu ya Andaa- Shiriki na Tafakari ni mkakati mwingine unaoweza kutumiwa ili kuboresha ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili kwa wanafunzi wa naojifunza kwenye shule za sekondari nchini Rwanda.

Mkakati huu unambidi mwanafunzi kujiandaa kwa kukumbuka aliyoyafundishwa kabla, kushiriki katika mchakato wa kufundisha na kujifunza wa somo analofundishwa na kutafakari kwa kujibu mwaswali yanayoonesha kwamba malengo ya kufundishia na kujifunzia yamefikiwa. (Sharon, 2021). Mbinu hii inaweza kutumiwa ifuatavyo:

Kabla ya kuanza kufundisha somo linalolenga kukuza stadi za kusoma na kuandika Kiswahili, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali ambayo yanaandaa akili zao kwa kujibu mwaswali yanayoweza kuwekwa kwenye chati au

ubaoni. Maswali anayoweza kuuliza ni kama vile: a) Unafikili utajifunza nini kwenye somo la leo? b) Je, unajua nini kuhusu somo utakalosoma leo? ch) Je, una swali gani kuhusu somo hilo utakalosoma leo? d) Je, unakusudia kupata uwezo upi baada ya kujifunza somo la leo? Baada ya kujibu maswali haya, kila mwanafunzi akiwa peke yake, mwalimu anaweza kuwakaza kwenye makundi ya watano watano na kuwaomba kuchangia na wenzao kwa njia ya usomaji majibu waliyotoa kuhusu mwaswali waliyoulizwa katika hatua ya maandlizi. Kwa hatua hii, wanafunzi watasaidiwa kuamsha akili yao na kiweka iwe tayari kwa ujifunzaji wa mambo mapya yanayolenga kuimarisha uandikaji na usomaji wa lugha ya Kiswahili.

Hatua ya pili, ni kushirikisha wanafunzi katika kuelewa kile anachokisoma na anachokiandika. Hapa, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi mazoezi ya ufahamu na utungaji; anaweza kuomba mwanafunzi yeyote kujaribu kutunga kifungu cha habari au insha kuhusu mada zinazohusiana na shughuli za kila siku kama vile biashara, siasa, uchumi, dini na nyinginezo. Baada ya utunguji mwalimu anaweza kuwaweka wanafunzi katika majozi na kuomba kila mwanafunzi kuhakiki kwa makini kifungu au insha iliyotungwa na mwenzake,

Hatua ya tatu nay a mwisho itakuwa ni kutafakari. Kwenye hatua hii kila mwanafunzi anasoma kwa makini kifungu au insha iliyotungwa na mwenzake kwa kudokeza mawazo makuu ya andiko, maswali ambayo anaweza kuuliza kuhusu andiko hilo, mawazo yake kuhusu andiko analosama na namna anavyoweza kuboresha kifungu au insha ili iweze kuwa muhimu na kuvutia zaidi.

Kwa kufuata utaratiu wa hapo juu, mwalimu atatimiza malengo ya kufundishia na kujifunzia stadi za kusoma na kuandika Kiswahili kwa kuwa wanafunzi watakuwa wamepewa maaria, stadi na maadili yanayohitajika katika usomaji na uandikaji.

Aidha, utumiaji wa mkakati wa Andaa- Shiriki na Tafakari  unaweza kukuza utamaduni wa kusoma na kuandika kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za

sekondari nchini Rwanda ambapo ukosefu wa utamaduni wa kusoma umekuwa changamoto inayokabili walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili kwa muda mrefu.

Kwa hiyo mbinu ya Andaa- Shiriki na Tafakari inafaa sana katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili kama inavyooneshwa na (Sharon, 2021:5) hapo chini.

> Prepare -Assist and reflect is a three-step strategy that helps students before, during, and after writing and reading. Teachers can use this strategy to equip evey student with effective skills that will enable him/her to become strong readers and writers.
>
> Andaa- Shiriki na Tafakari ni mkakati wa hatua tatu ambao husaidia wanafunzi kabla, wakati, na baada ya kujifunza stadi ya kuandika na kusoma. Walimu wanaweza kutumia mkakati huu kuwapa wanafunzi ujuzi unaofaa ambao utawawezesha kuwa wasomaji na wandishi mashuhuri (T.Y.).

Dondoo hili linathibitisha mchango wa Andaa- Shiriki na Tafakari katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika. Hivyo basi, walimu wanaofundisha Kiswahili kwenye shule za sekondari nchini Rwanda hasa kwenye wilaya ya Nyamagabe wanalazimika kutumia mkakati huu ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma na kuandika Kiswahili.

### 4.5.3 Utumiaji wa Usomaji na Uandikaji Gawizwa

Mkakati wa tatu unaweza kufaa sana katika uboreshaji stadi ya kusoma na kuandika Kiswahili katika kwa wanafunzi wanaojifunza kwenye shule za sekondari nchini Rwanda ni utumiaji wa usomaji na uandikaji gawizwa. Mkakati wa usomaji na uandikaji gawizwa unahusisha mwalimu kutoa mfano wa matamshi pamoja na tahajia bora na kuwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa

kusoma na kuandika kupitia mfano wa matamshi na tahajia bora waliopewa na mwalimu (Corrado, 1999).

Ili kufanikisha mkakati wa utumiaji wa usomaji na uandikaji gawizwa katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili kwenye shule za upili kwenye nchi ya Rwanda, mosi, mwalimu anaweza kuchagua riwaya au shairi na kulisomea wanafunzi mara zaidi ya mbili.

Pili, baada ya kusomea wanafunzi riwaya au shairi kwa mara ya mwisho, wanafunzi wanaweza kupewa mazoezi ya kusoma na kutunga riwaya au shairi, kuzungumzia msamiati mgumu upatikanao kwenye andiko, kuzungumzia lengo kuu la andiko, kudokeza mawazo makuu na kudhihirisha muundo na mtindo wa matini.

Tatu, mwalimu anaweza akakawaelekeza wanafunzi katika kuweka kisa cha riwaya au shairi katika maigizo ambayoyatawasidia wanafunzi kuelewa zaidi ujumbe uliopo kwenye riwaya au shairi. Uelewa wa ujumbe kutoka kwenye riwaya, shairi au andiko jingine, unasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa kuandika na kusoma Kiswahili. Uelewa huu pia, unaweza kuwapa wanafunzi uwezo wa kutunga rasimu mpya ya riwaya, shairi au andiko jingine.

Mwisho, mwalimu anaweza kumpa kila mwnafunzi nakala ndogo ya riwaya, shairi au aina nyingine ya insha na kuwaomba wafanye usomaji binafsi au kwa kushirikiana na wenzake shuleni, wazazi au walezi. Kwa kufuata utaratibu huu, kila mwanafunzi ataweza kubahatika kuwa na kifaa cha kusoma na  kuandika nah ii itakuza stadi za kusoma na kuandika Kiswahili kwa kuwa inaweza kushiriki katika utatuzi wa tatizo la ukosefu wa vifaa vya na kuandaika uliodhihirishwa kama changamoto inayokabili ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma na kuandika Kiswahil katika shule za sekondari wilayani Nyamagabe. Hivyo basi, utumiaji usomaji na uandikaji gawizwa ni muhimu katika ufundishajn na ujifunzaji wa

kusoma na kuandika Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanaungwa mkono na dondoo la hapo chini.

> Through shared reading and writing students are provided with opportunities to enjoy a variety of texts and to engage with the text afterwards through activities, such as discussion and writing (Corrado, 1999: 15).
>
> Kupitia mbinu ya usomaji na uandikaji gawizwa, wanafunzi wanapata bahati ya kufurahia matumizi ya maandishi anuwai na kujihusisha na maandishi baadaye kupitia shughuli, kama vile majadiliano na kuandika (T.Y.).

Kufuatana na yalioelezwa hapo juu, walimu wanalazimika kufuatilia mwongozo na utaratibu uliotolewa ili kuimarisha stadi za kuandika na kusoma Kiswahili katika shule za upili katika nchi ya Rwanda hasa kwenye wilaya ya Nyamagabe.

### 4.5.4 Utumiaji wa Ujenzi wa Maarifa

Ujifunzaji wa lugha ya pili ni mchakato ambamo wajifunzaji hujenga maana inayotegemea muktadha ambao ulijengwa. Hii inafanywa kwa kutazama mazingira na kujenga uwezo kwa kujiegemeza kwenye maarifa ya awali. Kwa hiyo, wanafunzi wa lugha ya pili, wanajifunza vizuri wakati wanapoingiriana hali halisi za jamii ambamo wanaishi inayohusiana na maarifa yao ya awali na malengo yao ambayo yanakuza utendaji huru na wa kujitegemea (Yung& Wilson, 2006).

Hivyo basi, mbinu ya ujenzi wa maarifa ni mbinu kufundishia na kujifunzia lugha ya ya pili ambapo mazingira halisi ya kufundishia na kujifunzia ayanatayarishwa ili wanafunzi washirikishwe ipasavyo katika kujenga maarifa, stadi na uwezo wa kusoma na kuandika kupitia uzoefu wao binafsi.

Katika utumiaji wa mkakati huu, mwalimu anashiriki kwenye mchakato wa kielimu kama mwelekezaji, mfasli na mrahisishaji. Chanzo cha kazi zote

zinazofanywa darasani, huwa ni mwanafunzi. Kwa hiyo, ili kufanikisha utumiaji wa mkakati wa ujenzi wa maarifa katika ufundishaji wa kufundisha kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za sekondari, kwanza, anaweza kuweka darasani vifaa vyote vinavyohitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma na kuandika Kiswahili. Vifaa hivi vinaweza kuwa vitabu, magazeti, majarida, riwaya, mashairi, Makala na aina nyingine za nyaraka. Kisha, mwalimu anaweza kuwasilisha malengo ya somo anarotarajia kufundisha na kuwaruhusu wanafunzi kugundua usuli na ukweli wa somo wao wenyewe kwa kutumia maelekezo na vifaa walivyopewa na mwalimu.

Aidha, mwalimu anaweza kuwapatia wanafunzi mwongozo mdogo unaolenga kuimarisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili. Mwongozo huu mdogo unaweza kuwafaa wanafunzi katika ujifunzaji kwa kuwasaidia kujibu haraka maswali waliyoulizwa. Hapa, mwalimu anatoa mwongozo mdogo akitambua kwamba kujaribu na kufanya makossa katika ujifunzaji si kitu kibaya baali ni sehemu ya uzoefu na ugunduzi. Kwa hiyo, katika mchakato wa kujaribu na kufanya makossa wanafunzi watakuza uzoefu wao na ugunduzi ambao utawawezesha kukuza stadi za kusoma na kuandika Kiswahili.

Hatimaye, kwenye mwisho wa somo, mwalimu anaweza kuwaweka wanafunzi pamoja darasani na kuwaomba kujadili lile walilologundua kuhusu somo somo la kusoma na kuandika Kiswahili walilofundisha. Pia, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi zoezi la mwisho la kuunganisha waliyogundua na ukweli wa maisha pamoja na uwezo wa awali waliokuwa nao.

Kwa kufuata utaratibu, walimu wanaweza kufundisha kusoma na kuandika Kiswahili kwa urahisi katika shule za sekondari nchini Rwanda kwa kuwa mbinu hii inahusisha ujifunzaji wa lugha ya pili na mazingira halisi kwa kushirikisha mwanafunzi katika mchakato wa elimu kama mtendaji na mwalimu kama mwelekezaji. Matokeo yaya yanaendana na mawazo ya mtafiti wa hapo chini.

> Knowledge Constructivism is associated with language teaching and learning situations as it assumes that learning is a process of structuring meaning in an active way and that a language teacher is to take the role of the facilitator rather than the knower (Philpo, 2014: 4).
>
> Ujenzi wa maarifa unahusishwa na hali ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kwa kuwa inadai kwamba ujifunzaji wa lugha ni mchakato wa kuunda uelewa kwa mbinu shirikishi na kwamba mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha anashiriki kama mwelekezaji badala ya kushiriki kama mjuzi (T.Y.).

Maelezo haya yanaonesha kwamba mwalimu anaposhiriki kama mwelekezaji, ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma na kuandika Kiswahili, utaimarika miongoni mwa wanafunzi kwa kuwa wanafunzi watashiriki katika ufundishaji na ujifunzaji ka watendaji nah ii itawasaidia kuunganisha nadharia kuhusu uomaji na uandishi na vitendo kamili. Ukweli huu unalingana na mhimili wa pili wa nadharia ya utamadunijamii ulioongoza utafiti huu. Mhimili husika unasisitiza kwamba ili ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili uzae matunda, ni lazima wanafunze wapewe nafazi ya kuweka matendoni waliyofundishwa darasani ili kutimiza lengo la kufanikisha mawasiliano. Kwa ufupi, sehemu hii imezungumzia mikakati inayoweza kutumiwa na walimu wanapofundisha stadi za kusoma pamoja na kuandika, sehemu inayofuata ni mchango wa MUU katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika kwenye shule za sekondari za nchi ya Rwanda.

### 4.6 Mchango wa MUU katika Ufundishaji wa Stadi Ya Kusoma na Kuandika

Lengo kuu la tasnifu hii lilikuwa kuchunguza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika MUU kwa wanafunzi wanaosoma kwenye shule za sekondari wilayani Nyamagabe Nchini Rwanda.  ndiyo yababu katika ukusanyaji wa data hatukusahau kukusanya taarifa zinazohusiana na mchango wa MUU

katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili kwenye shule za upili nchini Rwanda.

MUU ni mtaala uulioanzishwa katika nchi tofauti ili kukuza maarifa, stadi na mwenendo mwema kwa kuwawezesha wanafunzi kuhusisha waliyoyasoma shuleni na hali halisi ya maisha katika jamii (Ambai, 2018). Matokeo ya utafiti wetu yameonesha kwamba MUU una mchango mkubwa katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyamagabe nchini Rwanda.

Kwanza kabisa, MUU huwapa wanafunzi nafasi ya kushiriki katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma na kuandika na kuwaruhusu kuweka matendoni yale waliyojifunza darasani. Hii huimarisha stadi za kusoma na kuandika miongoni mwa wanafunzi. Hoja hii inathibitishwa na jibu lililotolewa kwa kujibu swali hili: "Mtaala Unaoegemea katika Uwezo (MUU) una mchango gani katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili?". Kwa kujibu swali hili, mwalimu mmoja alisema haya:

> MUU ni mtaala mzuri katika ufundishaji wa kusoma na kuandika Kiswahili. MUU unawashirikisha wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji na kuwabahatisha kuweka matendoni waliyosomeshwa (Mwalimu, 1).

Dondoo hili haliendi mbali na wazo la nadharia ya utamadunijamii ya Vygotsky, (1978) aoneshaye kwamba ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili ni vizuri nadharia ya za ujifunzaji wa lugha ziunganishwe na matend.

Pili, matokeo ya utafiti wetu yameonesha kuwa MUU unashiriki vikubwa katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili kwenye shule za sekondari katika wilaya ya Nyamagabe kwa kuwa MUU huwapa wanafunzi motisha inayowawezesha kutimiza malengo ya kielimu. Tunasema haya kutokana na jibu lililotolewa na mshiriki wa utafiti wa hapo chini.

Muu unawaomba walimu kutumia mbinu za ufundishaji zinazowavutia wanafunzi. Na kama mwalimu anatumia mbinu hizi kwa ufasaha, wanafunzi wanamudu funzo wanalofundishwa. Ndiyo sababu ninaona kuwa MUU unanifaa sana ninapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili kwa sababu unanipasa kutumia mbinu zinazoshirikisha wanafunzi na kuwafanya wafurahie kujifunza Kiswahili.

Matokeo ya utafiti wetu hayatofautiani na matokeo ya VVOB (2018: 24) kama inavyooneshwa hapo chini:

> The CBC is designed in a way that students feel excited about their schools. In CBC teaching and learning are centered on the learners, meaning that students now participate actively in the learning process and feel happy about studying.
>
> MUU umeundwa kwa mtindo ambao unawavutia wanafunzi katika madarasa yao. Katika MUU ufundishaji na ujifunzaji unaegemea kwenye mwanafunzi. Ni kumaanisha kwamba mwanafunzi anashiriki kiutendaji na kufurahia kujifunza (T.Y.)

Dondoo hili ninaonesha linathibitisha kuwa MUU una mchango mkubwa katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za upili kwenye wilaya ya Nyamagabe.

Tatu, MUU ni muhimu katika kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe kwa kuwa kupitia MUU wanafunzi wanapata nafasi ya kufanya utafiti binafsi na kugundua mambo mapya yanayowafaa wanaposoma na wanapoandika Kiswahili. Katika ukusanyaji tulitumia swali "Mtaala Unaoegemea katika Uwezo (MUU) una mchango gani katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya

kusoma na kuandika Kiswahili?". Dondoo la hapo chini linaonesha jibu lililotolewa na mhojiwa mmoja.

> MUU unatufaa sana tunapofundisha kusoma na kuandika Kiswahili. Kupitia MUU wanafunzi wanapata uwezo wa kugundua mambi mapya kupitia usomaji na uandishi binafsi (Mkuu wa Masomo 3).

Dondoo hili linaonesha kuwa MUU unashiriki katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili kwa kukuza uwezo wa utafiti na ugunduzi miongoni mwa wanafunzi katika wilaya ya Nyamagabe. Maelezo haya yanaendana na matokeo ya utafiti wa VVOB (2018) wanaosema kwamba MUU ni mtaala unaofaa katika elimu kwa kuwa unawapa wanafunzi wasaa wa kufanya utafiti na kugundua mambo mapya wao wenyewe ambayo yanawasaidia kukuza ujuzi, uwezo, stadi na maadili miongoni mwao.

Mwisho, matokeo ya utafiti wetu yameonesha kuwa MUU ukitumiwa vizuri, unaweza kushiriki katika utatuzi wa tatizo la uhaba wa vifaa vya kusoma na kuandikia ambalo linawakabili walimu wanaofundisha Kiswahili kwenyeshule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe. Ukweli huu huthibitishwa na jibu la hapo chini lililotolewa na mwalimu mmoja kwa kujibu swali kuhusu mchango wa MUU katika katika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili.

> Ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili unahitaji vifaa vingi sana. MUU unapotekelezwa, unalazimisha walimu kutumia vifaa hasa vya kiteknolojia ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji.kwa hiyo, ninaona kwamba MUU unanifaa kwa kuwa ninapotumia kompyuta zenye mtandao wa intaneti zinazopatikana shuleni kwetu, ingawaje hazitoshi, zinanifaa sana ninapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili (Mwalimu 5).

Dondoo hili linaonesha kuwa MUU unashiriki katika upatikanaji wa vifaa vya kusoma na kuandika vinavyofanikisha shughuli za kufundisha na kujifunza stadi za kusoma na kuandika Kiswahili kwenye shule za upili za wilaya ya Nyamagabe. Matokeo ya utafiti wetu yanalingana na matokeo ya utafiti wa Barman na Kornwar (2011) wanaosema kwamba kupitia teknolojia, MUU unawasidia walimu kuepuka changamoto ya ukosefu wa vitabu na baadhi ya zana zinazohitajika katika kufundisha na kujifunza somo lolote lile.

**4.7 Muhtasari wa Sura ya Nne**

Sura ya nne ilizungumzia uwasilishaji, uchanganuzi pamoja na mjadala wa matokeo ya utafiti uliofanyika, sura hii ilizungumzia utangulizi, uelewa wa walimu na wakuu wa masomo kuhusu lugha, stadi ya kusoma na kuandika na MUU, mbinu zinazotumiwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika, changamoto zinazokabili walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika, mikakati inayoweza kutumiwa na walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika na mchango wa MUU katika ufundishaji wa stadi ya kusoma na kuandikakatika shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe nchini Rwanda.

# SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sehemu ya tano ya utafiti wetu inaundwa na vipengele muhimu vitano ambavyo ni pamoja na utangulizi, muhtasari, ufaafu wa nadharia iliyotumika katika utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo mbalimbali tuliyoyapendekeza.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Tasinifu hii ililenga kutimiza malengo mahususi matatu ambayo ni kubainisha namna ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari wilayani Nyamagabe, kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika utekelezaji wa MUU kwa shule za sekondari wilayani Nyamagabe na kupendekeza mikakati inayoweza kutumiwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika kupitia MUU kwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Nyamagabe.

### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Utafiti wetu ulilenga kutimiza lengo mahususi la kwanza ambalo lilikuwa ni kubainisha namna ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari wilayani Nyamagabe. Matokeo ya utafiti yalionesha kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za sekondari za kwenye wilaya ya Nyamagabe ungali kwenye kiwango cha chini. Hili huthibitishwa na hoja zifuatazo:

Kwanza, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa walimu wa Kiswahili katika wilaya ya Nyamagabe hawanauelewa wa kutosha kuhusu lugha, stadi ya kusoma na kuandika pamoja MUU nah ii huwazuia kufundisha vilivyo stadi za kusoma na kuandika Kiswahili.

Vilevile, matokeo ya utatafiti yamedhihirisha kuwa walimu wa Kiswahili katika wilaya ya Nyamagabe wanatumia mbinu hafifu ambazo haziwezi kuwafaa wanapofundisha stadi ya kusoma na kuandika Kiswahili. Utumiaji wa mbinu hizi hafifu, unatokana na ukosefu wa uwezo wa wa kuandaa vilivyo maandlio ya mafunzo yanayolenga kukusa stadi ya kusoma na kuandika Kiswahili kwa wanafunzi.

Isitoshe, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma na kuandika Kiswahili wilayani Nyamagabe ungali kwenye kiwango cha chini kwa sababu walimu wa Kiswahili hawatilii mkazo stadi ya kusoma na kuandika Kiswahili wanapoandaa kazi na zana za kufundishia na kujifunzia kutokana kutoweza kuandaa masomo vilivyo kwa walimu wa shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe katika madarasa ya lugha.

### 5.2.2 Lengo Mahususi la Pili

Kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika utekelezaji wa MUU kwa shule za sekondari wilayani Nyamagabe lilikuwa lengo mahususi lililotizwa katika utafiti huu. Kwa kutimiza lengo hili kwanza, tuliegemeza utafiti wetu kwenye mhimili wa kwanza wa nadharia ya utamatunijamii unaohusu uunganishaji wa nadharia na vitendo katika kujifunza lugha ya pili na mhimili wa pili wa nadhari hii usemao kuwa, ili mtu aweze kujifunza lugha ya pili kwa ufanisi sharti mawasiliano yake yaunganishwe na shughuli mbalimbali za kijamii kama vile shughuli za kilimo, ufugaji, biashara, sherehe na mambo ya ibada. Pili, tulipitia matini zinazohusiana na lengo la pili la utafiti wetu na mwisho tulitumia mahojiano kati ya mtafiti na walimu na wakuu wa masomo ili kutimiza lengo husika. Changamoto zilizobainishwa ni pamoja na ukosefu wa utamaduni wa kuandika na kusoma, upatikanaji na ufanisi wa vifaa vinavyohitajika katika kusoma na kuandika,

ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi na uhaba wa walimu wenye uwezo.

### 5.2.3 Lengo Mahususi la Tatu

Utafiti wetu ililenga kutimiza lengo mahususi la tatu la kupendekeza mikakati inayoweza kutumiwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika kupitia MUU kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe. Kwa kutimiza lengo hili, tuegemeza utafiti wetu kwenye mahitaji ya MUU, mhimili wa kwanza wa nadharia ya utamadunijamii usemao kwamba ili mtu aweze kujifunza lugha ya pili kwa ufanisi ni sharti ujifunzaji wake uunganishwe na shughuli mbalimbali za kijamii kama vile shughuli za kilimo, ufugaji, biashara, sherehe na mambo mengine pamoja na mhimili wa pili na nadharia husika unaounganisha nadharia na matendo katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Mikakati tuliyopendekeza ni utumiaji wa TEHAMA, utumiaji wa Andaa-Shiriki na Tafakari, utumiaji wa usomaji na uandikaji gawizwa nautumiaji wa ujenzi wa maarifa.

Matokeo ya utafiti wetu yameonesha pia kuwa MUU una mchango mkubwa katika kufundisha na kujifunza wa Kiswahili kwa kuwa unawapa wanafunzi nafasi ya kushiriki katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma na kuandika na kuwaruhusu kuweka matendoni yale waliyojifunza darasani, unawapa wanafunzi nafasi ya kufanya utafiti binafsi na kugundua mambo mapya yanayowafaa wanaposoma na wanapoandika Kiswahili na unaweza kushiriki katika utatuzi wa tatizo la uhaba wa vifaa vya kusoma na kuandikia.

## 5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika

Utafiti ulioibua tasnifu hii uliongozwa na Nadharia ya Utamadunijamii iliyoasisiwa na Vygotsky mnamo mwaka wa 1997. Mhimili wa kwanza wa nadharia hii ni wa uunganishaji wa mawasiliano na shughuli za kijamii. Katika mhimili huu inasisitizwa kuwa, ili mtu aweze kujifunza lugha ya pili kwa ufanisi

sharti mawasiliano yake yaunganishwe na shughuli mbalimbali za kijamii kama vile shughuli za kilimo, ufugaji, biashara, sherehe na mambo ya ibada. Mhimili huu ulitusaidia kukamilisha lengo la kwanza la utafiti wetu la kubainisha namna ufundishaji pamoja na na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika kwa shule za sekondari kwenye wilaya ya Nyamagabe.

Mhimili wa pili wa nadharia ya utamadunijamii ni uunganishaji wa nadharia na vitendo katika kujifunza lugha ili kukidhi haja ya mawasiliano. Mhimili huu unadokeza ujifunzaji wa lugha ya pili katika mazingira rasmi ambapo kunakuwa na miongozo rasmi inayowekwa katika utendaji ili kuona ufaafu wake. Mhimili huu ulitufaa kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika utekelezaji wa MUU bali pia kupendekeza mikakati inayoweza kutumiwa na walimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kupitia MUU kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamagabe.

**5.4 Hitimisho**

Utafiti wetu umetimiza vilivyo lengo kuu na malengo mahususi yake. Tasnifu hii imeonesha kuwa ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za upili za wilaya ya Nyamagabe ungali kwenye kiwango cha chini kutokana na mbinu za ufundishaji anujifunzaji zinazotumiwa na walimu wanapofundisha Kiswahili pamoja ukosefu wa uwezo wa kuandaa vilivyo maandalio ya masomo kuhusu ukuzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili.

Tasnifu hii imeonesha kuwa walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili kwenye shule za upili za wilaya ya Nyamagabe wanakabiliwa na changamoto kadhaa wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili kama vile ukosefu wa utamaduni wa kuandika na kusoma, upatikanaji na ufanisi wa vifaa vinavyohitajika katika kusoma na kuandika, ukosefu wa motisha miongoni mwa

wanafunzi na uhaba wa walimu wenye uwezo. Ili kuepuka changamoto za hapo juu, utafiti wetu umependekeza mikakati inayoweza kutumiwa na walimu wanapofunndisha stadi za kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili ambayo ni utumiaji wa TEHAMA, utumiaji wa Andaa- Shiriki na Tafakari, utumiaji wa usomaji na uandikaji gawizwa na utumiaji wa ujenzi wa maarifa.

## 5.5 Mapendekezo

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Walimu Wanaofundisha Kiswahili

Matokeo ya utafiti wetu yameonesha kuwa kuna idadi kubwa ya walimu wa Kiswahili ambao hawana uwezo wa kutumia mbini zonazoweza kuwafaa katika ukuzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Kwa hiyo, walimu wa Kiswahili wanalazimika kukuza uwezo wao na kuboresha mbinu wanazozitumia wanapofundisha kwa kupitia MUU na nyaraka nyingine ili kujua mengi kuhusu ufundishaji na ujifunzaji stadi za kusoma na kuandika Kiswahili.

Pengine, tunapendekeza kuwa walimu wa Kiswahili nchini Rwanda wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika Kiswahili na lugha nyingine ni lazima watumie mbinu shirikishi ambazo humotisha wanafunzi na kukuza uwezo wao wa ugunduzi na utambuzi.

Walimu wa Kiswahili pia, wanalazimika kuhusisha TEHAMA wanapofundisha na wanalazimika kukuza maarifa, stadi na maadili miongoni mwa wanafunzi kwa kuwawezesha kutumia waliyoyasoma shuleni katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili jamii wanamoishi.

### 5.5.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu pamoja na Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda

Kutokana na kuwa matokeo ya utafiti yamedhihirisha kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili katika shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe ungali kwenye kiwango cha chini kutokana na kiwango cha uwezo cha chini kwa walimu wa Kiswahili, ukosefu wa vifaa vya kosoma na kuandikia na ukosefu wa walimu wa Kiswahili wenye uwezona mengineyo, Wizara ya Elimu kupitia Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda inalazimka kuandaa mafunzo ambayo yanalenga kuwafundisha walimu hasa wa Kiswahili mbinu bora za kufundishia stadi za lugha ya Kiswahili.

Aidha, Wizara ya Elimu na Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda ni lazima waungane mkono na wadau wengine wa sekta ya elimu ili kuhakikisha kuwa kila shule ya sekondari nchini Rwanda ina vifaa vya kusoma na kuandikia Kiswahili ambavyo vinaweza kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika Kiswahili.

Isitoshe, Wizara ya Elimu ya Rwanda inalazimika kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopewa nafasi za kusomea ufundishaji Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Rwanda na kuwaajiri wanapohitimu ili kutatua tatizo la uhaba wa walimu wenye uwezo linalokabili ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za Kiswahili nchini Rwanda.

### 5.5.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Kwanza, watafiti wengine watakaofanya utafiti, tunawapendekeza kufanya utafiti kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuongea Kiswahili kupitia MUU katiaka shule za sekondari au katika shule za ufundi nchini Rwanda.

Pengine, watafiti wengine wanalazimika kufanya utafiti unaolenga kuchunguza mchango wa TEHAMA katika kufundisha na kujifunza Kiswahili. Utafiti kama huu unakapofanyika, utafaa sana kwa sababu utadhihirisha namna ambavyo ufundishaji wa lugha ya Kiswahili unaweza kuboreshwa kupitia utumiaji wa TEHAMA.

Mwisho, watafiti wengine wanalazimika kufanya utafiti kuhusu MUU na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili ili kuonesha mchango wa MUU katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za sekondari hasa kwenye madarasa ya lugha nchini Rwanda.

### 5.5 Muhtasari wa Sura ya Tano

Kwa ujumla, sura ya nano ilizungumzia matokeo ya utafiti. Sura hii imeundwa na sehemu zifuatazo: utangulizi, muhtasari wa matokeo ya utafiti uliofanyika, ufaafu wa nadharia ya utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo mbalimbali.

# MAREJELEO


Adamson L. (2014) *Language, Literacy and Learning in Tanzanian Secondary Schools: an Ethnographic Perspective on the Student Experience*. Education Development Trust. Education Development Trust Highbridge House, 16–18 Duke Street, Reading, Berkshire RG1 4RU

Alderson, C. (2000). *Assessing Reading*. Cambridge: Cambridge University Press.

Ambei M.C. (2018).The Competency Based Curriculum Implementation: Appraisal from the Perspective of Teachers use of Resources. *International Journal of Trend in Scientific Research and Development - IJTSRD*, 2(4), 2456- 6470.

Babbie, E. (1992). *The Practice of Social Research* (Toleo la 6). Belmont: Wadsworth Publishers.

Barman, A., & Konwar, J. (2011). Competency Based curriculum in Higher Education: A necessity Grounded by Globalisation, *Revista Romaneasca Educatie, Multidimessionala*, (6), 7-15.

Bentolila, A. & Germain, B. (2005). *Apprendre à lire*: choix des langues et choix des méthode.

Bojovic, M. (2008). Development of reading skills in second language learning and teaching," *International Journal of Psychology*, vol. 43 (3/4), p. 223.

Brock-Utne, B. and Holmarsdottir, H.B. (2004) 'Language policies and practices in Tanzania and South Africa: problems and challenges'. *International Journal of Educational Development*, 24: 67-83.

Charmeux, E.( 2003). *No, deciphering is not reading*. (Not yet Published).

Chisholm, L. (2007). Diffusion of the National Qualifications Framework and Outcomes Based Education in Southern and Eastern Africa. *Comparative Education*, 43(2), 295-309. doi.org/10.1080/03050060701362631.

Choo, S. (2010). Writing through visual acts of reading: Incorporating visual aesthetics in integrated writing and reading tasks. *The High School Journal*, 93 (4), 166-176.

Choo, S. (2010). Writing through visual acts of reading: Incorporating visual aesthetics in integrated writing and reading tasks. *The High School Journal*, 93 (4), 166-176.

Cohen, L, Manion, M na Morrison, K. (2007*). Research methods in Education* (Toleo la 6). New York: Routledge Publisher.

Colmant, M. & Dos Santos, S. (2008). *Evolution des performances en lecture des élèves de CM1*. Résultats de l'étude internationale PIRLS. Note d'information 08.14 mars. Paris: Ministry of National Education, Division for Evaluation, Forecasting and Performance.

Corrado, C. (1999). Shared reading and writing: Directing the tour through text. *Perspectives in Education and Deafness, 17* (5), May/June, pp. 14-17

Dawson, C. (2002). *Practical Research Methods*. Magdalen Road Ox4IRE United Kingdom: Oxford University Press.

Delaney, Y.A. (2008). Investigating the reading-to-write construct. Education: *Journal of English for Academic Purposes, 7, 140-150.*

Dotson, V.M.; Kitner-Triolo, M.H.; Evans, M.H. & Zonderman, A.B. (2009, July). Effects of race and socioeconomic status on the relative influence of education and literacy on cognitive functioning. *Journal of the International Neuropsychological Society*, 15(4), 580-589. DOI: http://dx.doi.org/10.1017/ S1355617709090821.

Fema, B.M. (2003). Problem of Teaching English Language in NCE Programme. In *Azare Journal of Education*.4 (1):pp107-112.Fromkin, V. na Rodman, B. (1988), An Introduc tion to Language, Fort Worth, Holt Rinehart and Winston Inc.

Giasson, J. (2003) *La compréhension en lecture. Louvain-la-Neuve*: De Boeck (collection Pratiques pédagogiques).

Haigler, K.O.; Harlow, C.; O'Connor, P. & Campbell, A. (1994, December). *Literacy behind prison walls* (NCES 94102). Washington, DC: NCES. Retrieved from https://nces.ed.gov/ pubsearch/pubsinfo.asp?pubid=94102

Hall, A. H., A. Simpson, Y. Guo, and S. Wang. 2015. "Examining the Effects of Preschool Writing Instruction on Emergent Literacy Skills: A Systematic Review of the Literature." *Literacy Research and Instruction* 54 (2): 115–34.

Harmer, J. (2004). *How to Teach Writing*. England: Longman.
Harmer, J. (2007). *The Practice of English Language Teaching*. England: Longman.
Hatier (2017).*L'ouvrage dirigé par Maryse Bianco et Laurent Lima, Comment enseigner la compréhension en lecture*.

Jonson, R. (2001);."Trained Language Teacher". *Linguistic Quarterly* 57-102.

Kershner, R., 2000. Developing Student Teachers' Understanding of Strategies for Teaching Sen Children. *Education Today*, 4(50): 31-39.

Khakasa, L.S. (2018). *Mikakati ya Kufundisha Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi katika Shule za Msingi za Kaunti ya Kakamega Nchini Kenya*. (Haijachapishwa).

Kirn, E. and Hartmann, P. (2016). Interactions Reading I. New York, McGraw. *Hill Education*, (3) 2-240.

Klimova, Blanca Frydrychova (2013), "The Importance of Writing. *Indian Journal of Research*. (2), 9-11.

Kombo, D.K. na Tromp, D.L. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology*: Methods and Techniques. New Delh, India: New Age International (P).

Leticja, P. G. (2015). Factors that Affect Effective Planning Skills of the Teacher in the Classrooms. *Academic Journal of Interdisciplinary Studies*, (4) 560-564

Likisa, K. D. (2018). Challenges and Prospects of Competency-based Education: The Case of Adama Science and Technology University Alumni Students and Hawas TVET College, Adama, Ethiopia. *The Journal of Competency based Education*, 3(2),1-7.

Malik, S., Gasana, J., Board, R. E., Raab, E., Cha, K., & Goldenberg, C. (2014). *Literacy Boost*. Rwanda.

Marianne, T. (2017). *Les pratiques effectives d'acculturation à l'écrit en classe de CP: impact sur les eprésentations des élèves et sur l'apprentissage du lire-écrire*. Linguistique. Université Grenoble. NNT: 2017GREAL022.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Melor, M. Y., Norazah, N. , Hadi, S., Choo H. S. & Mohamed, A. E. (2013) *Pros and Cons of Using ICT in Teaching ESL Reading and Writing.*

Mligo, E.S. (2012). *Jifunze Utafiti*: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).

Mutale M. I. & Malambo Y. K. (2019). Understanding a Competency-Based Curriculum and Education: The Zambian Perspective by the University of Zambia *Journal of Lexicography and Terminology*, 3(1), 1006- 108.

Nasser, O. & Majid, V. (2011). Motivation, attitude, and language learning. *International Conference on Education and Educational Psychology*, (29) 994 – 1000.

Nkurunziza, F. C. (2012). *Reading Culture in Rwandan community: Benefits and Challenges*. (Haijachapishwa)

Nunan, D. (2003). *Practical English Language Teaching*. New York: The McGraw Hill.

Nzima, I. (2016) *Tutors' Interpretations of Competence-Based Curriculum in Tanzania*: Implications for Practice in Teacher Education. Journal of Education of the University of Dar es Salaam.

Okoba, B. W. (2008). *Kuchunguza Ufundishaji wa Kusoma kwa Sauti katika Madarasa ya Kwanza, Pili na Tatu katika Shule za Msingi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Park, H. & Kyei, P. (2007). *Literacy gaps by educational attainment*: A comparative study of 19 countries (PARC Working Paper Series, WPS 07-12). Retrieved from http://repository. upenn.edu/parc_working_papers/1

Pearson, J. (2003). Information and Communications Technologies and Teacher Education in Australia. *Technology, Pedagogy and Education*, 12(1), 39-58.

Philpo, J. (2014). *Constructivism: Its Implications for Language Teaching and Second-Language Acquisition*. University of Dar es Salaam Press.

REB. (2015). *Competence Based Curriculum: Summary of Curriculum Framework Pre-Primary to Upper Secondary 2015*. World Core Communication Limited.

Rosiana, K. L. (2014). *Teaching Literacy in Fiji Classrooms*: Curriculum Innovation at Levuka Public Primary .School of Education, University of the South Pacific, Suva.

Rubagumya, C.M. (1990). *Language in education in Africa*: a Tanzanian perspective. Clevedon: Multilingual Matters.

Rugemalira, J.M. (2005) 'Theoretical and practical challenges in a Tanzanian English medium primary school'. *Africa & Asia*, 5: 66-84.

Ruterana, P. C. (2012). *The Making of a Reading Society*: Developing a Culture of Reading in Rwanda, (Unpublished Doctoral Thesis) linkoping University Educational Sciences, Linkoping.

Ruterana. P, C (2012). Enhancing the Culture of Reading in Rwanda: Reflections by Students in Tertiary Institutions, *The Journal of Pan African Studies*, (5) 2-25.

Sandra J. & Rod J. (2016).*Literacy in France Country Report Children and Adolescents*: The European Literacy Policy Network (ELINET)

Sharon, L. (2018). *Strategies for Teaching Reading & Writing Across Content Areas*. Retrieved from https://study.com/academy/lesson/strategies-for-teaching-reading-writing-across-content-areas.html.

TET. (2005).). *Ukuzaji mitaala na Kunasihi*. Dar es Salaam: KIUTA.

TET. (2013). *Moduli ya kujifunzia somo la ualimu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Urbanova, L. and Oakland, A. (2002). *Uvod do anglicke stylistiky*. *Pedagogická fakulta*. ISBN 80-86598-33-0

VVOB (2018). Implementing CBC: Successes and Challenges. *Urunana rw'abarezi*. (1) 1-32.

Vygotsky, L. (1978) Mind Society. *The Development of Higher Psychological Process*. Cole, M, Steiner, V, Scriber, S na Souberman, E (Wah.). E. Combridge, Massachuttes, & London: Havard University Press.

Wambui, M. (2011). *Ufundishaji wa Kusoma kwa Sauti Katika Madarasa ya Chini Katika Shule za Msingi Tarafa ya Gatanga*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi.

Yang, L. & Wilson, K. (2006). *Second-language classroom reading: A social constructivist approach. 5 th Anniversary Special Issue,* 6(3), 364-372.

**1. Mwongozo wa Mahojiano kwa Walimu wa Kiswahili**

1. Nini maana ya stadi za kuandika?

   What is the meaning of writing skills?

2. Nini maana ya stadi za kusoma?

   What is the meaning of reading skills?

3. Nini maana ya Mtaala Unaoegemea katika Uwezo?

   What do you understand by Competence Based Curriculum?

4. Unatumia mbinu gani unapofundisha stadi ya kuandika kwa wanafunzi wako?
   Indicate some strategies that you use to enhance writing skills among your students.

5. Ni mbinu gani ambazo walimu huzitumia wanapofundisha stadi ya kusoma kwa wanafunzi kwenye shule yenu?

   Indicate some strategies that you use to enhance reading skills among your students.

6. Kama mwalimu wa Kiswahili, ni changamoto zipi unazokabiliana nazo unapofundisha stadi ya kuandika?

   As a Kiswahili teacher, what challenges do you face when teaching writing skills?

7. Kama mwalimu wa Kiswahili, ni changamoto zipi unazokabiliana nazo unapofundisha stadi ya kusoma?

   As a Kiswahili teacher, what challenges do you face when teaching reading skills?

8. Kama mwalimu wa Kiswahili, pendekeza mikakati inayoweza kutumiwa ili kuepuka changamoto zinazokabili ufundishaji wa stadi ya kuandika.

As a Kiswahili teacher, suggest strategies that can be used to overcome challenges faced in teaching reading skills.

9. Mtaala Unaoegemea katika Uwezo una mchango gani katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuandika Kiswahili?

   What is the contribution of Competence Based Curriculum in teaching and learning Kiswahili writing skills?

10. Mtaala Unaoegemea katika Uwezo una mchango gani katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma Kiswahili?

    What is the contribution of Competence Based Curriculum in teaching and learning Kiswahili reading skills?

**II. Mwongozo wa Mahojiano kwa Wakuu wa Masomo**

1. Nini maana ya Mtaala Unaoegemea katika Uwezo?

   What do you understand by Competence Based Curriculum?

2. Ni mbinu gani ambazo walimu huzitumia wanapofundisha stadi ya kuandika kwa wanafunzi kwenye shule yenu?

   Indicate some strategies that are used by teachers to enhance writing skills among students.

3. Ni mbinu gani ambazo walimu huzitumia wanapofundisha stadi ya kusoma kwa wanfunzi kwenye shule yenu?

   Indicate some strategies that are used by teachers to enhance reading skills among students.

4. Ni changamoto zipi wanazokabiliana nazo walimu wanapofundisha stadi ya kuandika kwenye shule yenu?

As a Head of Studies, what challenges faced by teachers when teaching writing skills?

5. Ni changamoto zipi wanazokabiliana nazo walimu wanapofundisha stadi ya kusoma kwenye shule yenu?

   As a Head of Studies, what challenges faced by teachers when teaching reading skills?

6. Kama Mkuu wa Masomo, pendekeza mikakati inayoweza kutumiwa na walimu ili kuepuka changamoto zinazokabili ufundishaji wa stadi ya kuandika.

   As a Head of Studies, suggest strategies that can be used to overcome challenges faced in teaching writing skills.

7. Kama Mkuu wa Masomo, pendekeza mikakati inayoweza kutumiwa na walimu ili kuepuka changamoto zinazokabili ufundishaji wa stadi ya kusoma.

   As a Head of Studies, suggest strategies that can be used to overcome challenges faced in teaching reading skills.

8. Mtaala Unaoegemea katika Uwezo una mchango gani katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuandika?

   What is the contribution of Competence Based Curriculum in teaching and learning Kiswahili writing skills?

9. Mtaala Unaoegemea katika Uwezo una mchango gani katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma?

   What is the contribution of Competence Based Curriculum in teaching and learning Kiswahili reading skills?

## 3. Kibali cha Kukusaya Data

UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

**RESEARCH AND INNOVATION UNIT**

Rukara, 13th July2022
Ref: 03/DRI-CE/103/EN/gi/2022

**The Mayor**
**Nyamagabe district**
**Southern Province**
**Rwanda**

**Re: Research recommendation letter for Mrs. Concessa MUKASHEMA**

On behalf of the University of Rwanda-College of Education (UR-CE), I am pleased to introduce **Mrs Concessa Mukashema**, a post-graduate student at the School of Education of UR-CE. Mrs Mukashema is writing a thesis on: **"Teaching and Learning of writing and reading skills in competency-based curriculum among Kiswahili students in secondary schools of Nyamagabe district"** to complete her Master of Education in Kiswahili Education. She wishes to assess the teaching and learning of Kiswahili's writing and reading skills through a competence Based Curriculum (CBC). This research will involve Kiswahili teachers and S4 students learning Literature-Kinyarwanda-Kiswahili (LKK) in secondary schools. Thus, she requests permission to collect data from the selected secondary schools from Nyamagabe district.

Mrs Mukashema's research project passed successfully through an internal collegial ethical process. Thus, the University of Rwanda-College of Education: Directorate of Research and Innovation confirms that this research adheres to ethical standards and principles. Therefore, we kindly request you to accord her your cooperation in this research.

We very much hope to get your cooperation.

Yours sincerely.

COLLEGE OF EDUCATION
RESEARCH AND INNOVATION

**Digitally signed by**
**UR (Rukara, Directorate of Research & Innovation)**
**Date: 2022.07.13**
**Time: 13:05:10 +2'00**

**Assoc. Prof. Eugene Ndabaga**
Director of Research and Innovation
University of Rwanda-College of Education
E-mail: ndabagav@yahoo.ie
Mobile: +250788308862

**Cc:**

- Principal, UR-CE
- Postgraduate Program Coordinator, School of Education
- Dr. Patrice Ntawigira (Supervisor)

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw    P.O. Box: 55 Rwamagana    WEBSITE: www.ur.ac.rw